TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA

# MTAALA WA SHULE YA JUNIA

# KISWAHILI

## GREDI YA NANE

DRAFT

Toleo la Kwanza 2023

Iliyorekebishwa 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN: 978-9914-43-796-6**

Kimechapishwa na kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

## DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU

Serikali ya Kenya imejitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera kuhusu elimu, mafunzo na utafiti yanatimiza malengo ya Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya Kenya 2030, Sera ya Mtaala ya Kitaifa 2019, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na Mikataba ya Kikanda na ya Kimataifa ambayo Kenya ni mshirika. Katika kutimiza lengo la Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu imefanikiwa kutekeleza hatua kwa hatua Mtaala wa Kiumilisi katika viwango vya Chekechea, Shule ya Msingi na katika Daraja ya Awali ya Shule za Upili.

Utekelezwaji wa Mtaala wa kiumilisi, unahusisha, kuangalia mara kwa mara vile unaendelea kutekelezwa ili kutathmini utekelezwaji wake. Miaka mitano baada ya kutekelezwa kwake, tathmini tamati ya utekelezwaji ulifanywa katika shule za msingi ili kubainisha ufanisi wake kama inavyopendekezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF). Serikali ya Kenya iliunda Tume ya Rais ya Elimu ya kushughulikia masuala mbalimbali, yanayoathiri sekta ya elimu nchini mwaka wa 2022. Tume hii ilitoa mapendekezo mbalimbali, yaliyochangia marekebisho ya mtaala. Mapendekezo ya tume hii, ripoti za tathmini, tathmini tamati zilizofanywa, mapendekezo kutoka kwa washikadau, na wale wanaotekeleza mtaala yalisababisha hatua ya kufanya marekebisho katika mtaala pamoja na kuchunguza upya masomo yaliyopendekezwa. Mitaala ya Gredi ya 8 inaendeleza umilisi walioupata wanafunzi kufikia mwisho wa Gredi ya 7. Aidha, inatoa fursa kwa wanafunzi kuendelea kutalii na kukuza uwezo wao wanapojiandaa kujiunga na Daraja ya Awali ya Shule za Upili.

Mtaala huu unaeleza Malengo ya Elimu ya Kitaifa, kauli kiini, matokeo ya kijumla na maalum yanayotarajiwa kwa kila somo pamoja na mada na mada ndogo. Mtaala huu pia unabainisha shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa, maswali dadisi yaliyopendekezwa, umilisi wa kimsingi unaokuzwa, masuala mtambuko, maadili, shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji na vigezo na viwango vya kuzingatia katika kutathmini.

Ni matumaini yangu kuwa, mashirika yote ya serikali na washikadau wengine wa elimu watatumia mtaala kuandaa utekelezaji fanifu na wenye tija wa Mtaala wa Kiumilisi.

**MHE. EZEKIEL OMBAKI MACHOGU, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU**
**WIZARA YA ELIMU**

## DIBAJI YA KATIBU MKUU

Wizara ya Elimu imetekeleza Mtaala wa Kiumilisi ulioanza mwaka wa 2019. Gredi ya 8 ndiyo kiwango cha pili cha Daraja ya Awali Shule za Upili katika mpangilio mpya wa elimu.

Mtaala wa Gredi ya 8 uliofanyiwa marekebisho, unaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi kutoka Gredi ya 7.Sifa kuu ya daraja hii ni mtaala mpana unaomwezesha mwanafunzi kutalii talanta, hamu na uwezo wake kabla ya kuchagua mkondo wa masomo katika Daraja ya Juu Shule za Upili. Hili ni muhimu sana katika kutimiza ruwaza na lengo la mabadiliko ya mtaala yanayoendelea kama ilivyoelezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 wenye mada: *Kuelekea kufikia Elimu Bora, Faafu na Jumuishi na Mafunzo kwa Maendeleo Endelevu Nchini Kenya*. Mswada huu unafafanua mabadiliko kutoka kwa mtaala unaolenga kupokeza maarifa hadi mtaala unaolenga *kukuza uwezo wa kila mwanafunzi.* Kwa hivyo, mtaala wa Gredi ya 8 unakusudiwa kuimarisha ukuaji wa mwanafunzi katika umilisi wa kimsingi wa Mtaala wa Kiumilisi ambao ni: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu, uraia, ujuzi wa kidijitali, hamu ya ujifunzaji na kujiamini.

Mtaala huu unatoa shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa husishi na tofautishi kuambatana na mada ndogo mbalimbali na vipengele vingine vya Mtaala wa Kiumilisi. Mtaala pia unapendekeza nyenzo za kufundishia pamoja na mbinu anuwai za kutathmini. Inatarajiwa kuwa mtaala huu utawaongoza walimu kikamilifu kuwaelekeza wanafunzi kufikia matokeo yanayotarajiwa katika Gredi ya 8 na kuwaandaa kuingia katika gredi inayofuata bila tatizo.Vilevile, ni matumaini yangu kuwa walimu watautumia mtaala huu kuufanya ujifunzaji kuwa wa kuvutia, kuchangamsha na wenye kufurahisha.

**Dkt. BELIO KIPSANG', CBS**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

DRAFT

**SHUKRANI**

Sheria Nambari 4 ya 2013 (iliyorekebishwa 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) inaipa mamlaka Taasisi kukuza mitaala na nyenzo za utekelezaji mtaala kwa elimu ya msingi na taasisi za elimu na mafunzo. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote cha elimu huhusisha utafiti wa kina, ulinganishi wa kimataifa na uhusishaji mkubwa wa wadau. Kupitia kwa mchakato uliopangwa kikamilifu na wa mashauriano, KICD ilibuni Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) 2017,ambao unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

KICD hupata ufadhili kutoka kwa Serikali ya Kenya ili kuwezesha ufikiaji kikamilifu wa majukumu na utekelezaji wa mipango ya serikali na sekta za Wizara ya Elimu. Taasisi pia inapata msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo unaolenga miradi mahususi. Mtaala wa Gredi ya 9 uliofanyiwa marekebisho, umeandaliwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mpango wa *Kenya Primary Education Equity in Learning Programme (KPEELP*) ulio chini ya uelekezi wa Wizara ya Elimu. Kwa hivyo, Taasisi inatoa shukrani za dhati kwa msaada kutoka kwa Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Elimu na washirika wengine wa maendeleo kwa sera na msaada wa mali na mikakati. Taasisi inatoa shukrani za kipekee kwa Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu katika Idara ya Serikali ya Mafunzo ya Awali na Elimu ya Msingi.

Tungependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wakufunzi walioshiriki kama wanajopo katika ukuzaji wa mitaala. Nashukuru pia Mashirika Huru ya Serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali kwa michango yao katika kuuandaa Mtaala wa Gredi ya 9. Kwa mintarafu hii, tunatambua msaada wa Afisa Mkuu Mtendaji wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza la Kitaifa la Mitihani nchini Kenya (KNEC) kwa usaidizi wao katika mchakato mzima wa kuuandaa mtaala. Mwisho, tunamshukuru Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) na wanachama wengine wa Baraza kwa uelekezi wao wa mara kwa mara katika mchakato huu.

Tunawahakikishia walimu wote, wazazi na wadau wengine kuwa mtaala huu utaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya 8 na uandaaji wa wanafunzi kwa Gredi ya 9.

**PROF. CHARLES O. ONG'ONDO, PhD, MBS**
**MKURUGENZI/OFISA MTENDAJI MKUU**
**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

## YALIYOMO

DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU ..... I
DIBAJI YA KATIBU MKUU ..... II
SHUKRANI ..... III
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ..... VI
MGAO WA VIPINDI ..... VIII
MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA KIWANGO CHA KATI CHA ELIMU YA MSINGI ..... IX
KAULI KIINI ..... IX
MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA SHULE YA JUNIA ..... X
MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO ..... XI
MWONGOZO WA KUTUMIA VITABU VYA KUSOMA SHULE YA JUNIA ..... XV
1.0 USAFI WA SEHEMU ZA UMMA ..... 1
2.0 MATUMIZI YAFAAYO YA DAWA ..... 10
3.0 DHIKI ZINAZOKUMBA WANYAMA ..... 18
4.0 MATUMIZI BORA YA MALIASILI ..... 26
5.0 MAJUKUMU YA KIJINSIA ..... 34
6.0 USALAMA NYUMBANI ..... 42
7.0 KUHUDUMIA WENYE MAHITAJI MAALUM ..... 50

DRAFT

**8.0 UHALIFU WA MTANDAONI** ... **58**
**9.0 MAJUKUMU YA MNUNUZI** ... **67**
**10.0 KUKABILIANA NA HISIA** ... **77**
**11.0 HAKI ZA WATOTO** ... **86**
**12.0 MAGONJWA YASIYOAMBUKIZWA** ... **95**
**13.0 HESHIMA KWA TAMADUNI ZA WENGINE** ... **103**
**14.0 KUWEKA AKIBA** ... **111**
**15.0 MAADILI YA KIJAMII** ... **120**
**MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA** ... **129**
**MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI** ... **137**
**TATHMINI YA MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI** ... **138**
**MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI** ... **140**

DRAFT

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.
   **a) Mahitaji ya kijamii**
   Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.
   **b) Mahitaji ya kiuchumi**
   Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.
   **c) Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
   Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda. Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

DRAFT

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

**MGAO WA VIPINDI**

| | **Somo** | **Vipindi kwa wiki (Dakika 40 kwa kipindi)** |
|---|---|---|
| 1. | English | 5 |
| 2. | Kiswahili/KSL | 4 |
| 3. | Mathematics | 5 |
| 4. | Integrated Science | 5 |
| 5. | Social Studies | 4 |
| 6. | Religious Studies | 4 |
| 7. | Pre-Technical Studies | 4 |
| 8. | Agriculture | 4 |
| 9. | Creative Arts and Sports | 5 |
| | Pastoral/Religious Instructional Programme | 1* |
| | **Jumla** | **40 +1*** |

DRAFT

## MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA KIWANGO CHA KATI CHA ELIMU YA MSINGI

Kufikia mwisho wa kiwango cha kati cha elimu mwanafunzi aweze:

1. kutumia ujuzi wa kusoma na kuandika, ujuzi wa kuhesabu na kufikiri kimantiki ifaavyo katika kujieleza
2. kuwasiliana kikamilifu katika miktadha mbalimbali
3. kudhihirisha ujuzi wa kijamii, pamoja na tunu za kiimani na kimaadili kwa ajili ya mahusiano mema
4. kutalii, kubadilisha, kusimamia na kutunza mazingira ifaavyo kwa ajili ya ujifunzaji na maendeleo endelevu
5. kufanya usafi, kufuata kanuni zifaazo za usafi na lishe ili kuimarisha afya
6. kudhihirisha mienendo ya kimaadili na kuonyesha uraia mwema kama wajibu wa kiraia
7. kuonyesha ridhaa kwa mirathi mingi na tofauti ya kitamaduni nchini ili kuleta mshikamano wa kimahusiano
8. kudhibiti masuala mtambuko katika jamii ifaavyo
9. kutumia ujuzi wa kidijitali ifaavyo kwa madhumuni ya mawasiliano na ujifunzaji.

## KAULI KIINI

Somo la Kiswahili litampa mwanafunzi wa Shule ya Junia umilisi katika shughuli za kila siku. Umilisi huu utajengea haiba na uwezo wake wa kuwasiliana na kuhusiana katika jamii, kitaifa na kimataifa. Aidha, litamwendeleza kielimu na kumwandaa kwa ulimwengu wa kazi. Somo hili litampa mwanafunzi hamasa ya kumudu na kufurahia lugha na fasihi kwa kuzihusisha na tajiriba na mazingira yake. Hali kadhalika, litampa mwanafunzi maarifa ya kijamii na kitamaduni. Mwanafunzi ataweza kujieleza na vilevile kupata fursa ya kutoa huduma kwa jamii.

**MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA SHULE YA JUNIA**

Kufikia mwisho wa Shule ya Junia, mwanafunzi aweze:

1. kujieleza ipasavyo kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa njia ya maandishi na mazungumzo
2. kuwasiliana ipasavyo katika miktadha mbalimbali ya kijamii
3. kujenga desturi ya kusoma na kufasiri maandishi kwa ufasaha
4. kutumia lugha kiubunifu kusimulia na kuandika tungo mbalimbali
5. kushiriki katika shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji
6. kutumia teknolojia ipasavyo katika ujifunzaji na mawasiliano ili kukuza ujuzi wa kidijitali
7. kutumia maadili yanayohitajika maishani kupitia stadi za lugha ya Kiswahili
8. kufurahia na kuthamini lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi, ya taifa na kimataifa.

DRAFT

## MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO

| Mada | Mada Ndogo | Idadi ya Vipindi Vilivyopendekezwa |
|---|---|---|
| **KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | 1.1.1 Kusikiliza na Kujibu: Mahojiano | 2 |
| | 2.1.1 Kusikiliza kwa Kina; sauti /g/ na /gh/ | 2 |
| | 3.1.1 Hadithi: Mighani | 2 |
| | 4.1.1 Hadithi: Visasili | 2 |
| | 5.1.1 Kusikiliza Maagizo | 2 |
| | 6.1.1 Kusikiliza kwa Kufasiri | 2 |
| | 7.1.1 Usikilizaji Husishi | 2 |
| | 8.1.1 Uzungumzaji wa Papo kwa Hapo | 2 |
| | 9.1.1 Kusikiliza kwa Kina: Sauti **//ch** na **/sh/** | 2 |
| | 10.1.1 Hadithi: Hurafa na Hekaya | 2 |
| | 11.1.1 Kuzungumza kwa Kutumia Vidokezo vya Hoja | 2 |
| | 12.1.1 Kusikiliza kwa Makini | 2 |
| | 13.1.1 Hadithi: Wahusika | 2 |
| | 14.1.1 Hadithi: Matumizi ya Lugha | 2 |
| | 15.1.1 Usikilizaji Husishi | 2 |
| **KUSOMA** | 1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Simulizi | 2 |
| | 2.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini ya kujichagulia | 2 |
| | 3.2.1 Kusoma kwa Kina: Tamthilia | 2 |
| | 4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |

DRAFT

| | | |
|---|---|---|
| | 5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 6.2.1 Kusoma kwa Kina: Maudhui na Dhamira | 2 |
| | 7 .2.1 Ufupisho | 2 |
| | 8.2.1 Kusoma kwa Kina: Mandhari na Ploti | 2 |
| | 9.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**:** Kifungu cha Kushawishi | 2 |
| | 10.2.1 Kusoma kwa Kina: Wahusika katika Tamthilia | 2 |
| | 11.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini ya kujichagulia | 2 |
| | 12.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| | 13.2.1 Kusoma kwa Kina: Mbinu za Lugha | 2 |
| | 14.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 15.2.1 Ufupisho | 2 |
| **KUANDIKA** | 1.3.1 Viakifishi: Alama ya hisi na Ritifaa | 2 |
| | 2.3.1 Barua ya Kirafiki: Barua ya kirafiki ya kutoa shukrani | 2 |
| | 3.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |
| | 4.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |
| | 5.3.1 Insha ya Maelekezo | 2 |
| | 6.3.1 Insha za Kubuni: Insha ya mdokezo | 2 |
| | 7.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 8.3.1 Viakifishi: Mtajo na mshazari | 2 |
| | 9.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |
| | 10.3.1 Barua ya Kuomba Msaada | 2 |

DRAFT

| | | |
|---|---|---|
| | 11.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 12.3.1 Insha za Kiuamilifu: Hotuba ya kutoa ufafanuzi | 2 |
| | 13.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 14.3.1 Insha za Maelekezo | 2 |
| | 15.3.1 Baruapepe ya Kiofisi | 2 |
| **SARUFI** | 1.4.1 Viwakilishi: Viwakilishi vya Nafsi, Viwalikishi Vionyeshi na Viwakilishi vya Idadi | 2 |
| | 2.4.1 Viwakilishi: Viwalikishi vya Sifa, Viwalikishi vya Pekee na Viwalikishi Viulizi | 2 |
| | 3.4.1 Viwakilishi: Vimilikishi na Visisitizi | 2 |
| | 4.4.1 Nyakati na Hali: Hali ya mazoea na Hali timilifu | 2 |
| | 5.4.1 Nyakati na Hali: Wakati uliopita hali timilifu na Wakati ujao hali timilifu | 2 |
| | 6.4.1 Vivumishi vya Sifa na Viashiria | 2 |
| | 7.4.1 Vivumishi Vimilikishi na vya Idadi | 2 |
| | 8.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi: Ngeli ya I-ZI Ngeli ya I-I | 2 |
| | 9.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi: Ngeli ya U-U na U-YA | 2 |
| | 10.4.1 Vinyume vya Vitenzi na Vielezi | 2 |
| | 11.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi: Kauli ya: Kutendeka, Kutendewa na Kutendatenda | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 12.4.1 Aina za Sentensi: Sentensi changamano | 2 |
| | 13.4.1 Ukanushaji kwa Kuzingatia Hali: Hali ya mazoea na Hali timilifu | 2 |
| | 14.4.1 Udogo wa Nomino | 2 |
| | 15.4.1 Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa | 2 |
| **Jumla ya vipindi** | | 120 |

**Kumbuka:** Idadi ya vipindi vilivyopendekezwa kwa kila mada ndogo vinaweza kuwa vichache au vingi kutegemea na muktadha.

DRAFT

## MWONGOZO WA KUTUMIA VITABU VYA KUSOMA SHULE YA JUNIA

### Lengo la Vitabu vya Kusoma katika Shule ya Junia

Utanzu ulioteuliwa wa kusomwa katika Gredi ya Nane ni wa Tamthilia. Matokeo yanayotarajiwa:

a) kukuza jadi ya usomaji miongoni mwa wanafunzi jambo ambalo ni muhimu miongoni mwa wanafunzi katika maisha yao ya ujifunzaji,
b) kuwaandaa wanafunzi kusoma fasihi katika somo la Kiswahili katika mkondo wa Sayansi ya Jamii katika Shule ya Juu,
c) kuwatanguliza wanafunzi katika vipengele vya kimsingi vya fasihi ambavyo ni muhimu katika maisha ya kila siku tukijua kwamba wengine watasoma fasihi katika Shule ya Juu.

### Kufunza vitabu vya Kusoma katika Shule ya Junia

**Wanafunzi katika shule ya Junia:**

a) wataongozwa kusoma vitabu mbalimbali ili kuwapa nafasi ya kuingiliana na dhana na stadi katika mtaala. Hali hii itawaweka katika hali ya kupata stadi za kuzungumza, kusikiliza, kusoma, kuandika, sarufi mwanzoni,
b) wanatarajiwa kwamba ataingiliana na tanzu mbalimbali ili kuwa na kuwa na uzoevu na dhana za kimsingi za fasihi ili kujiburudisha na pia kukuza mazoea ya usomaji,
c) hawapaswi kushirikishwa katika uhakiki wa kazi za fasihi kwa undani.

Ni muhimu kukumbuka kuwa ni vitabu tu vilivyoidhinishwa na KICD vinavyopaswa kusomwa kulingana na viwango lengwa.

### Tathmini ya Vitabu vya Kusoma

Kama inavyopendekezwa katika mtaala, tathmini endelevu na tamati haipaswi kuegemea vitabu vyovyote teule. Hii ni kwa sababu vitabu hivi vya kusoma SIO vitabu teule vya fasihi au *setbooks* kama vinavyojulikana. Tathmini inapaswa kuwa wazi na ya vipengele vya kimsingi kulenga dhana za kimsingi kama zinavyoelekezwa katika mtaala. Zaidi ya hayo, tathmini inapaswa kufanywa kwa njia ambayo kila mwanafunzi atakuwa na nafasi sawa bila kujali ni kitabu gani ambacho mwanafunzi amesoma.

## 1.0 USAFI WA SEHEMU ZA UMMA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1 Kusikiliza na Kujibu**<br><br>*Mahojiano*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mahojiano,<br>b) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kujibu mahojiano,<br>c) kutumia vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mahojiano ipasavyo,<br>d) kuchangamkia kushiriki mahojiano katika miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mahojiano,<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kujibu mahojiano,<br>• kusikiliza mahojiano kuhusu suala lengwa katika kifaa cha kidijitali na kutambua vipengele vya kusikiliza na kujibu mahojiano vilivyozingatiwa,<br>• kuwawasilishia wenzake vipengele vya kusikiliza na kujibu mahojiano vilivyozingatiwa katika mahojiano aliyosikiliza katika kifaa cha kidijitali,<br>• kushiriki mahojiano kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake, mzazi au mlezi kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya kusikiliza na kujibu mahojiano. | Je, ni vipengele vipi vinavyofaa kuzingatiwa katika kusikiliza mahojiano? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia vipengele vifaavyo kujieleza katika mahojiano akiwa na wenzake.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kama vile simu, redio au kanda za sauti kusikilizia mahojiano mbalimbali ili kutambua vipengele vya usikilizaji faafu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapopendekeza vipengele sahihi vya kuzingatia na kuvitumia katika kusikiliza na kujibu mahojiano.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki katika mahojiano na kujieleza kwa ukakamavu. Pia anapochangia katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mahojiano na wenzake, mzazi au mlezi na kujifunza njia bora za kusikiliza na kujibu mahojiano. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kuzungumza katika mahojiano bila kuwakata kauli.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji na kushirikiana na wenzake. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Masuala ya afya na mazingira: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza na kujibu mahojiano aliyojifunza katika somo la Kiwahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa sehemu za umma na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu** *Kifungu cha Simulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha simulizi,<br>b) kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha simulizi,<br>c) kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha simulizi,<br>d) kueleza maana ya msamiati katika kifungu cha simulizi,<br>e) kuchangamkia kujibu maswali ya ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu cha simulizi kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>• kudondoa habari mahususi *(k.v. nani? nini? wapi? lini?)* katika kifungu cha simulizi,<br>• kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha simulizi,<br>• kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha simulizi alichosoma,<br>• kutambua msamiati (*k.v. maneno na nahau)* katika kifungu cha simulizi na kuueleza kwa kutumia kamusi,<br>• kusoma vifungu vya simulizi mtandaoni au kwenye vitabu kuhusu suala lengwa,<br>• kutambua na kueleza maana ya msamiati wa usafi wa sehemu za umma kulingana na muktadha wa matumizi katika vifungu vya | 1. Je, tunapataje habari mahususi katika kifungu cha simulizi?<br>2. Je, ni mambo gani yanayoweza kukusaidia kuelewa kifungu cha simulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | simulizi alivyosoma mtandaoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi sentensi kuhusu usafi wa sehemu za umma kisha wajadiliane umuhimu wa kudumisha usafi wa mazingira ya umma. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili na kudondoa habari mahususi kutoka kwenye kifungu alichosoma.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotumia msamiati wa suala lengwa kwa usahihi katika muktadha maalum.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapobashiri na kufasiri kutokana na kifungu cha ufahamu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kusoma vifungu kuhusu suala lengwa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji. Pia anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa.
- Masuala ya afya na mazingira: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa na kuzingatia ujumbe.

DRAFT

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kifungu cha simulizi, na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa sehemu za umma na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Viakifishi**<br><br>• *Alama ya hisi*<br>• *Ritifaa*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya alama ya hisi na ritifaa katika matini,<br>b) kutumia alama ya hisi na ritifaa ipasavyo katika matini,<br>c) kuonea fahari matumizi yafaayo ya alama ya hisi na ritifaa katika matini. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua alama ya hisi na ritifaa katika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kwenye matini andishi na za kidijitali,<br>● kuandika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kuhusu kwa kutumia alama ya hisi na ritifaa ipasavyo kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>● kuandika kwenye tarakilishi, kifungu kifupi kuhusu kwa kutumia alama ya hisi na ritifaa ipasavyo na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili wakitolee maoni,<br>● kusahihisha kifungu kuhusu suala lengwa ambacho hakijatumia alama ya hisi na ritifaa ipasavyo,<br>● kuwasomea wenzake kifungu alichoandika na kuwataka waandike maneno, sentensi au vifungu vinavyofaa kutumia alama ya hisi na ritifaa, | 1. Je, alama ya hisi huonyesha hisia zipi?<br>2. Je, alama ya ritifaa hutumiwa vipi katika maandishi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumwonyesha mzazi, mlezi au mwenzake maneno, vifungu vya maneno au sentensi zenye alama ya hisi na ritifaa alizotunga ili atoe maoni yake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuwasomea kifungu alichokiandika.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika kifungu na kukisambaza mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya alama ya hisi na ritifaa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomwonyesha mzazi au mlezi wake maneno, vifungu vya maneno na sentensi ambazo zina alama ya hisi na ritifaa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa.
- Masuala ya afya na mazingira: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia alama ya hisi na ritifaa ipasavyo.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya alama hisi na ritifaa aliyojifunza katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa sehemu za umma na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Viwakilishi**<br>• *Viwakilishi vya Nafsi*,<br>• *Viwalikishi Vionyeshi*<br>• *Viwakilishi vya Idadi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi katika matini<br>b) kutumia viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi yafaayo ya viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kuchopoa viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi katika kapu maneno, chati, mti maneno au katika tarakilishi,<br>● kutaja viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi,<br>● kutambua viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi katika sentensi au vifungu kwenye vitabu au tarakilishi kwa kuvipigia mstari au kuvikolezea wino,<br>● kujaza nafasi katika sentensi au vifungu akitumia viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi ipasavyo<br>● kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia viwakilishi vya nafsi, vionyeshi/viashiria na vya idadi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la usafi wa sehemu za umma, | Viwakilishi vina umuhimu gani katika mawasiliano? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kumsomea mzazi au mlezi wake sentensi au vifungu alivyotunga ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia viwakilishi mbalimbali kuwatungia wenzake sentensi na kuwashirikisha kutunga sentensi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua viwakilishi mbalimbali.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia viwakilishi mbalimbali.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**
- Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapoandika sentensi kuhusu suala lengwa.
- Masuala ya afya na mazingira: mwanafunzi anapoandika sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia viwakilishi mbalimbali.

**Uhusiano na masomo mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya viwakilishi katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa sehemu za umma na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

DRAFT

## 2.0 MATUMIZI YAFAAYO YA DAWA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>*Sauti /**g**/ na /**gh**/*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti /**g/** na **/gh/** katika silabi na maneno,<br>b) kutamka sauti **/g/** na /**gh/** ipasavyo katika silabi na maneno,<br>c) kutumia maneno yenye sauti /**g/** na **/gh/** ipasavyo katika matini ili kuyatofautisha kimatamshi,<br>d) kuchangamkia matamshi bora ya sauti **/g/** na /**gh/** katika mazungumzo ya kawaida. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua sauti /**g/** na /**gh**/ katika maneno na silabi,<br>● kusikiliza maneno, sentensi au vitanzandimi vinavyohusisha sauti /**g**/ na /**gh/** katika kifaa cha kidijitali na kutambua sauti hizo,<br>● kutafuta maneno yenye sauti /**g**/ na /**gh/** katika matini andishi au za kidijitali na kuyatamka ipasavyo,<br>● kutunga sentensi akitumia maneno yenye sauti /**g/** na /**gh/** na kuziwasilisha darasani ili wenzake wazisikilize na kuzitathmini,<br>● kushiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /**g**/ na /**gh/**. | Ni maneno yapi yaliyo na sauti /**g/** na /**gh/**? |

| |
| --- |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza vitanza ndimi vyenye sauti lengwa.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi akitumia maneno yenye sauti lengwa.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti lengwa na anapochangia katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji na kutunza vifaa vya kidijitali alivyotumia.<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Afya ya mtu binafsi: mawanafunzi anapotunga sentensi akizingatia suala lengwa.<br>● Elimu ya afya ya kujikinga: mawanafunzi anapotumia maneno yanayohusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora aliyojifunza katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi yafaayo ya dawa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza ujumbe wa matini aliyosoma,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia,<br>c) kutumia ipasavyo msamiati unaotokana na matini aliyosoma,<br>d) kujenga mazoea ya kusoma matini za miktadha mbalimbali ili kupanua mawanda ya fikra. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuteua matini kuhusu suala linalomvutia,<br>• kusoma matini aliyojichagulia na kutambua vipengele vyake muhimu,<br>• kueleza ujumbe wa matini aliyoisoma,<br>• kuweka rekodi ya aliyosoma kwa kuyanakili katika kijitabu,<br>• kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia<br>• kutumia kamusi kutafuta maana za maneno asiyoyajua,<br>• kutunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma,<br>• kusakura mtandaoni na kujichagulia matini zaidi kuhusu suala lengwa kisha aisome,<br>• kuwawasilishia wenzake kwa kifupi alichojifunza kutokana na matini aliyoisoma mtandaoni. | 1. Unazingatia nini unapochagua matini ya kusoma?<br>2. Unapataje ujumbe katika matini uliyoisoma? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi na pia kutoa muhtasari wa matini aliyosoma.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia msamiati aliojifunza.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi. |
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafuta na kusoma matini. Pia anapotafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma matini ya kujichagulia kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposoma matini ya kujichagulia kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa mapana katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu usomaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi yafaayo ya dawa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Barua ya Kirafiki**<br><br>*Barua ya kirafiki ya kutoa shukrani*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza umuhimu wa barua ya kirafiki ya kutoa shukrani,<br>b) kutambua vipengele vya kimuundo vya barua ya kirafiki ya kutoa shukrani,<br>c) kuandika barua ya kirafiki ya kutoa shukrani kwa kuzingatia ujumbe, lugha na muundo ipasavyo,<br>d) kukuza mazoea ya kuandika barua ya kirafiki ya kutoa shukrani katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza umuhimu wa kuandika barua ya kirafiki ya kutoa shukrani kuhusu masuala mbalimbali,<br>• kutambua ujumbe unaoafiki barua ya kirafiki ya kutoa shukrani,<br>• kutambua lugha inayofaa kwa uandishi wa barua ya kirafiki ya kutoa shukrani,<br>• kujadili vipengele vya kimuundo vya barua ya kirafiki ya kutoa shukrani (*k.v. anwani ya mwandishi*, *tarehe*,),<br>• kuandika barua ya kirafiki ya kutoa shukrani daftarini au kwenye tarakilishi,<br>• kuwasilisha insha yake darasani au kumsambazia mwenzake kupitia mtandaoni ili aitolee maoni,<br>• kumwandikia mzazi, mlezi au mwenzake barua ya kirafiki ya kutoa shukrani na kuiwasilisha darasani. | 1. Je, ni mambo gani yanayoweza kukufanya uandike barua ya kirafiki ya kutoa shukrani?<br>2. Barua ya kirafiki ya kutoa shukrani huwa na vipengele gani? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili vipengele vya barua ya kirafiki ya

DRAFT

| |
|---|
| kutoa shukrani.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika barua na kuisambaza mtandaoni.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika barua ya kirafiki ya kutoa shukrani. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapoandika barua ya kirafiki kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapoandika barua kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa barua ya kirafiki ya kutoa shukrani katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu uandishi huo katika somo la English<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi yafaayo ya dawa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Viwakilishi**<br><br>• *Viwalikishi vya Sifa,*<br>• *Viwalikishi vya Pekee*<br>• *Viwalikishi Viulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi katika matini,<br>b) kutumia viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi ifaavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuchopoa viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi katika kapu maneno, kadi maneno, chati au katika tarakilishi,<br>• kutaja viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi,<br>• kutambua viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi katika sentensi au vifungu kwenye vitabu au tarakilishi kwa kuvipigia mstari au kuvikolezea wino,<br>• kujaza nafasi zilizoachwa katika sentensi na vifungu kwa kutumia viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi vifaavyo,<br>• kutunga sentensi au vifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia viwakilishi vya sifa, vya pekee na viuliziakizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la matumizi yafaayo ya dawa,<br>• kumtungia mzazi, mlezi au mwenzake | 1. Kuna tofauti gani kati ya viwakilishi vya sifa na vivumishi vya sifa?<br>2. Viwakilishi vya vya pekee hutumiwa kwa namna gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | sentensi zinazotumia viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi na kuzituma mtandaoni ili wenzake na mwalimu wazitolee maoni. | |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi mtandaoni.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia viwakilishi vya sifa, vya pekee na viulizi. | | | | |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. | | | | |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapotunga sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. | | | | |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya viwakilishi katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi yafaayo ya dawa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. | | | | |

DRAFT

## 3.0 DHIKI ZINAZOKUMBA WANYAMA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Hadithi**<br><br>*Mighani*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza dhana ya mighani ili kuipambanua,<br>b) kujadili vipengele vya kuzingatia katika uwasilishaji wa mighani,<br>c) kujadili ujumbe na lugha katika mighani,<br>d) kusimulia mighani kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji wa mighani,<br>e) kuchangamkia kushiriki katika uwasilishaji wa mighani katika miktadha mbalimbali ya kijamii. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya mighani,<br>• kutafiri na kueleza sifa za mighani,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika uwasilishaji wa mighani,<br>• kushiriki na wenzake kujadili ujumbe na lugha katika mighani aliyosikiliza ikitambwa na wenzake, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijiali kama vile kinasasauti,<br>• kusikiliza mighani ikisimuliwa katika vifaa vya kidijitali au kutoka kwa mgeni mwalikwa na kubainisha sifa na vipengele vya uwasilishaji vilivyozingatiwa,<br>• kusimulia mighani kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uwasilishaji, | Je, unaposimulia mighani unafaa kuzingatia vipengele gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuwasilishia mzazi, mlezi au mwenzake mighani aliyotafitia katika jamii yake na kujadili ujumbe husika. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusimulia mighani na kufafanua sifa za mighani.
- Uwazaji kina: mwanafunzi anapochanganua ujumbe na lugha katika mighani.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika kutafiti kuhusu mighani ya jamii yake akiwa na mzazi au mlezi wake.
- Uraia: mwanafunzi anapotafitia na kuthamini mighani katika jamii yake.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake.
- Uzalendo: mwanafunzi anaposimulia mighani ya jamii yake na kuionea fahari. Pia mwanafunzi anapojifunza kujitolea mhanga, kuitumikia jamii yake kutokana na matendo ya jagina katika mighani.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anaposimulia hadithi kuhusu suala lengwa.
- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapowazia kuhusu umuhimu wa wanyama.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mighani katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dhiki zinazokumba wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2. Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>*Tamthilia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya tamthilia ili kuipambanua,<br>b) kujadili sifa za tamthilia kama utanzu wa fasihi andishi,<br>c) kuchangamkia usomaji wa tamthilia ili kukuza stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya tamthilia,<br>• kutafiti maktabani au mtandaoni kuhusu sifa za tamthilia,<br>• kuwawasilishia wenzake utafiti wake darasani au kuwasambazia mtandaoni ili wautolee maoni,<br>• kusoma tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu na kutambua sifa zake,<br>• kuwasilishia mzazi, mlezi au mwenzake sifa za tamthilia aliyosoma ili azitolee maoni. | Je, tamthilia uliyowahi kusoma ilikuwa inahusu nini? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotangamana na wenzake na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji na kujadili sifa za tamthilia.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kutafiti kuhusu maana na sifa za tamthilia.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojitolea kufanya utafiti maktabani au mtandaoni kuhusu maana na sifa za tamthilia. | | | | |

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafiti kuhusu maana na sifa za tamthilia maktabani na mtandaoni. Pia anapowawasilishia wenzake darasani.<br>• Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni yake kwa upendo kuhusu uwasilishaji wa wenzake. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anaposoma tamthilia, mtazamo wake wa wa ulimwengu unaweza kubadilika na kukua.<br>• Masuala mtambuko mbalimbali kutegemea maudhui ya tamthilia. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha usomaji wa tamthilia katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu usomaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dhiki zinazokumba wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Insha ya masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kubaini wazo moja kuu la insha ya masimulizi atakayoandika,<br>b) kuandika insha ya masimulizi inayoendeleza wazo moja kuu katika kila aya,<br>c) kufurahia kuandika insha za masimulizi katika maisha ya kila siku akizingatia ujumbe uliotegemezwa kwenye wazo moja kuu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua wazo moja kuu la simulizi kwenye matini andishi na za kidijitali au katika kielelezo cha insha za kubuni,<br>• kuandika insha ya masimulizi kuhusu suala lengwa akizingatia wazo moja kuu,<br>• kuliendeleza wazo moja kuu katika kila aya kupitia kwa wahusika katika simulizi,<br>• kuandika kwenye tarakilishi, insha ya kubuni kuhusu suala lengwa akizingatia wazo moja kuu na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili waitolee maoni,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika na kuwataka kutambua wazo moja kuu. | Je, ni vipengele vipi vya kimsingi utakavyozingatia unapoandika insha ya kubuni? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika insha na kuisambaza mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha kwa kuzingatia wazo moja kuu.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha aliyoandika.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapoandika insha ya kubuni kuhusu suala lengwa.<br>• Elimu ya fedha: mwanafunzi anapoandika insha ya kubuni kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dhiki zinazokumba wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Viwakilishi**<br>• *Viwakilishi Vimilikishi*<br>• *Viwakilishi Visisitizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viwakilishi vimilikishi na visisitizi katika matini,<br>b) kutumia viwakilishi vimilikishi na visisitizi ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia viwakilishi vimilikishi na visisitizi katika sentensi na vifungu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kuchopoa viwakilishi vimilikishi na visisitizi katika kapu la maneno, orodha ya maneno, sentensi, vifungu au katika tarakilishi,<br>• kutaja viwakilishi vimilikishi na visisitizi,<br>• kutambua viwakilishi vimilikishi na visisitizi katika orodha ya maneno, sentensi, vifungu kwenye vitabu au tarakilishi kwa kuvipigia mstari au kuvikolezea wino,<br>• kujaza nafasi kwenye sentensi au vifungu kwa kutumia viwakilishi vimilikishi na visisitizi ipasavyo,<br>• kutunga sentensi au vifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia viwakilishi vimilikishi na visisitizi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la dhiki zinazokumba wanyama,<br>• kumsomea mzazi, mlezi au | 1. Unazingatia nini unapotumia viwakilishi vimilikishi?<br>2. Je, viwakilishi visisitizi vina muhimu gani katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mwenzake sentensi zinazotumia viwakilishi vimilikishi na visisitizi ili azitolee maoni. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotajia wenzake viwakilishi vimilikishi na visisitizi.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia viwakilishi vimilikishi na visisitizi.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua viwakilishi vimilikishi na visisitizi na kuvitungia sentensi sahihi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji, pia anapojitolea kufanya kazimradi. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapoandika sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya viwakilishi katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la dhiki zinazokumba wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

## 4.0 MATUMIZI BORA YA MALIASILI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Hadithi**<br><br>*Visasili*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza dhana ya visasili ili kuibanisha,<br>b) kujadili vipengele vya kimsingi katika uwasilishaji wa visasili,<br>c) kuwasilisha visasili kwa kuzingatia uwasilishaji ufaao,<br>d) kufurahia uchambuzi na uwasilishaji wa visasili ili kujenga umahiri katika fasihi simulizi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya visasili,<br>• kufanya utafiti maktabani na mtandaoni kuhusu sifa za visasili,<br>• kuwawasilishia wenzake matokeo ya utafiti wake wa sifa za visasili ili wazijadili,<br>• kujadili vipengele vya kimsingi katika uwasilishaji wa visasili (*k.v. ujumbe, wahusika na mbinu za lugha*),<br>• kusikiliza visasili katika vifaa vya kidijitali au kutoka kwa mgeni mwalikwa na kubainisha vipengele vya kimsingi vya uwasilishaji wa visasili,<br>• kusimulia visasili kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi vya visasili,<br>• kujadili na mzazi au mlezi kuhusu visasili katika jamii yake,<br>• kusimulia visasili akiwa na mzazi, mlezi au mwenzake akizingatia vipengele vya kimsingi vya | 1. Je, uwasilishaji wa hadithi ya visasili huzingatia vipengele gani?<br>2. Visasili vina sifa gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | uwasilishaji. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kusimulia visasili kwenye kikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza visasili mbalimbali.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anaposimulia visasili.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki kusimulia visasili na mzazi, mlezi au mwenzake. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika majadiliano ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapowasilisha visasili kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapowasilisha visasili kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.<br>• Umaskini: mwanafunzi anapowazia jinsi matumizi yafaayo ya maliasili yanaweesha kupunguza umaskini. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya visasili katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi bora ya maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Social Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) Kutambua vipengele vya kusoma kwa ufasaha ili kuvibainisha,<br>b) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>d) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>e) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>f) kuchangamkia kusoma kifungu kwa kuzingatia vipengele vya usomaji. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha,<br>• kutazama na kusikiliza video inayoonyesha usomaji fasaha wa makala *(k.v. hotuba, habari,)*,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali akizingatia matamshi bora,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno sahihi yasiyopungua 100 kwa dakika*),<br>• kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo,<br>• kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa,<br>• kushirikiana na mzazi au mlezi kusoma makala akizingatia vipengele vya usomaji bora. | 1. Je, kusoma kwa ufasaha kuna umuhimu gani?<br>2. Unaposoma kifungu ni mambo yapi unayozingatia ili kufanikisha usomaji kwa ufasaha? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kujadiliana kuhusu vipengele vya kusoma kwa ufasaha.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa ufasaha.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotumia ishara zifaazo wakati wa kusoma kifungu.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kusoma. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzajiwanapojadili vipengele vya usomaji bora.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika mjadala wakati wa shughuli ya ujifunzaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuwasomea wenzake kifungu.<br>• Umoja:  mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili vipengele vya usomaji bora. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufasaha katika somo la Kiswahili na usomaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi bora ya maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Insha ya masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mbinu za lugha katika insha ya masimulizi,<br>b) kujadili umuhimu wa mbinu za lugha katika insha za masimulizi,<br>c) kujadili wahusika na mandhari katika insha za masimulizi,<br>d) kuandika insha ya masimulizi akizingatia mbinu za lugha, wahusika wanaobainika na mandhari ifaavyo,<br>e) kufurahia kuandika insha ya masimulizi akizingatia lugha, wahusika na mandhari ifaavyo ili kukuza ubunifu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua mbinu za lugha *(k.v. tashbihi, sitiari, nahau,)* katika vielelezo vya insha ya masimulizi,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa lugha ya kiubunifu katika vielelezo vya insha za masimulizi,<br>• kutafiti maktabani au mtandaoni kuhusu umuhimu wa mbinu za lugha katika insha ya masimulizi,<br>• kuwasilisha utafiti wake darasani ili kujadiliana na wenzake,<br>• kujadili na wenzake wahusika na mandhari katika vielelezo vya insha za masimulizi kutoka kwenye maandishi au vifaa vya kidijitali,<br>• kuandika insha ya masimulizi akitumia lugha kiubunifu na kuwabainisha wahusika na mandhari akizingatia suala lengwa,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika ili waitathmini,<br>• kumsomea mzazi, mlezi au mwenzake | 1. Je, ni vipengele vipi vya kimsingi utakavyozingatia unapoandika insha ya masimulizi?<br>2. Mbinu za lugha zina umuhimu gani katika uandishi wa insha ya masimulizi? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>kielelezo cha insha ya masimulizi ili aitolee maoni.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya insha ya masimulizi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutafiti kuhusu mbinu za lugha.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi wa insha ya masimulizi.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi bora ya maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Social Studies.</td></tr>
</table>

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Nyakati na Hali**<br><br>• *Hali ya mazoea*<br>• *Hali timilifu*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hali ya mazoea na timilifu,<br>b) kubainisha vitenzi vilivyo katika hali ya mazoea na timilifu katika matini,<br>c) kutumia hali ya mazoea na timilifu ipasavyo katika matini,<br>d) kufurahia kutumia hali ya mazoea na timilifu ipasavyo ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya hali ya mazoea na timilifu,<br>• kusoma kifungu na kutambua hali iliyotumiwa,<br>• kuchagua vitenzi vinavyoashiria hali ya mazoea na timilifu katika chati, sentensi, vifungu, na tarakilishi,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia hali ya mazoea na timilifu ipasavyo,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi daftarini mwake au katika kifaa cha kidjitali kwa kutumia hali ya mazoea na timilifu akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la matumizi bora ya maliasili,<br>• kuwasomea wenzake au kuwasambazia mtandaoni kazi yake ili ili waitolee maoni,<br>• kumwasilishia mzazi, mlezi au mwenzake sentensi alizotunga katika hali ya mazoea na timilifu. | 1. Je, unapotaka kuonyesha kwamba jambo hutokea mara kwa mara utatumia viambishi vipi?<br>2. Je, unapotaka kuonyesha kwamba jambo limefanyika na kukamilika utatumia viambishi vipi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua hali ya mazoea na hali timilifu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu hali ya mazoea na hali timilifu.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua hali ya mazoea na hali timilifu na kuzitungia sentensi sahihi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya mazingira na tabia nchi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa hasa kuhusu suala maliasili katika mazingira yake.<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa na kuwazia kuhusu matumizi ya maliasili. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nyakati na hali katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi bora ya maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Social Studies. |

DRAFT

## 5.0 MAJUKUMU YA KIJINSIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Kusikiliza Maagizo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maagizo ili kuyapambanua,<br>b) kutambua maagizo katika miktadha mbalimbali,<br>c) kujadili sifa za kimsingi za maagizo yafaayo,<br>d) kutoa na kupokea maagizo ipasavyo,<br>e) kuchangamkia kutoa na kufuata maagizo ifaavyo katika miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya maagizo ili kuipambanua,<br>• kubainisha maagizo miongoni mwa kauli zilizoandikwa katika kadi, kapu maneno au vifaa vya kidijitali,<br>• kutambua maagizo kutoka kwenye kitabu, chati au vifaa vya kidijitali,<br>• kujadili na wenzake sifa za kimsingi za maagizo yafaayo,<br>• kutafiti maktabani au mtandaoni kuhusu sifa za maagizo na kuwawasilishia wenzake darasani wazitathmini,<br>• kuigiza utoaji na uitikiaji wa maagizo mbalimbali kwa uwazi,<br>• kujadiliana na wenzake kuhusu aina mbalimbali za maagizo kulingana na miktadha ya jamii zao,<br>• kusikiliza maagizo ya aina | 1. Je, kwa nini mtu hupewa maagizo?<br>2. Maagizo ambayo umewahi kupewa yalikusaidia vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mbalimbali yanayotolewa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kutaja maagizo yaliyomo,<br>• kuandaa maagizo na kisha kuyawasilisha darasani ili yajadiliwe na wenzake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kujadili sifa za maagizo.
- Uraia: mwanafunzi anapojifunza kudumisha mahusiano mema kwa kufuata maagizo. Pia anapojifunza kuheshimu majukumu ya kijinsia.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza maagizo akiwa na wenzake.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anapoigiza maagizo na wenzake wakizingatia suala lengwa.
- Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu aina mbalimbali za maagizo kulingana na miktadha ya jamii.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maagizo katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu,<br>b) kueleza maana ya msamiati kulingana na muktadha wa kifungu cha ufahamu,<br>c) kuchangamkia kusoma kwa ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali,<br>• kueleza habari za kifungu kwa ufupi,<br>• kuchopoa msamiati wa suala lengwa na kuutia kwenye kapu la maneno,<br>• kueleza maana za maneno kulingana na muktadha wa matumizi katika matini,<br>• kusakura vifungu vya ufahamu kuhusu suala lengwa kwenye vifaa vya kidijitali,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu kifupi kwa sauti na kueleza habari husika kwa ufupi. | Ni kwa njia gani tunaweza kudondoa habari mahususi kutokana na kifungu cha ufahamu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapotumia msamiati wa suala lengwa katika muktadha maalum.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoeleza maana ya msamiati kulingana na muktadha maalum.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma makala mbalimbali kuhusu suala lengwa. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo na wenzake. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Masuala ya jinsia: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufahamu katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Insha ya Maelekezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua insha ya maelekezo katika matini,<br>b) kujadili sifa za insha ya maelekezo,<br>c) kuandika insha ya maelekezo akizingatia anwani na mpangilio ufaao,<br>d) kufurahia kuandika insha za maelekezo maishani. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya insha ya maelekezo,<br>• kusoma kwenye kamusi au kifaa cha kidijitali maana ya insha ya maelekezo,<br>• kutambua aina za insha za maelekezo kwenye maandishi au vifaa vya kidijitali,<br>• kubainisha sifa za insha ya maelekezo kwa kuzingatia vielelezo vya insha kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali (*k.v. usahihi wa habari*, *mpangilio wa maelezo wenye mantiki*, *lugha sahili*),<br>• kushiriki kuandaa mpangilio ufaao wa hatua za insha ya maelekezo,<br>• kuandika insha ya maelekezo akizingatia vipengele vyake muhimu (*k.v. anwani na mpangilio mwafaka wa hatua*) huku akitumia vipengele vya lugha, | Je, ni mambo gani unayozingatia unapoandika insha ya maelekezo? |

DRAFT

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili kuhusu maana na aina za insha za maelekezo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusakura maana ya insha ya maelekezo.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelekezo akizingatia vipengele vyake muhimu.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha aliyoandika.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>● Masuala ya jinsia: mwanafunzi anapoandika insha ya maelekezo kuhusu suala lengwa.<br>● Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelekezo katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.</td></tr>
</table>

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Nyakati na Hali**<br><br>• *Wakati uliopita hali timilifu*<br>• *Wakati ujao hali timilifu*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu ili kuzipambanua,<br>b) kutambua viambishi vya wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu katika matini,<br>c) kutumia wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu ipasavyo katika matini,<br>d) kuchangamkia kutumia wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu ipasavyo ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu,<br>● kutambua viambishi vya wakati uliopita hali timilifu *(li, me)* na wakati ujao hali timilifu *(ta, me)*,<br>● kutenga vitenzi vilivyo katika wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu kutoka kwenye chati au mti maneno,<br>● kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu ipasavyo,<br>● kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia wakati uliopita hali timilifu na wakati ujao hali timilifu akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la majukumu ya kijinsia,<br>● kuandika kifungu kifupi kwenye kifaa cha kidijitali na kuwasambazia wenzake mtandaoni ili wakibadilishe | Kwa nini ni muhimu kujifunza nyakati na hali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | katika nyakati na hali lengwa. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kutoa mchango wake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika kifungu kifupi na kuwasambazia wenzake mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi na vifungu sahihi kuhusu nyakati na hali lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nyakati na hali na kuzitungia sentensi sahihi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizotunga kwa kutumia nyakati na hali lengwa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anapotunga sentensi mbalimbali kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya wakati uliopita hali timilifu na ujao hali timilifu katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

## 6.0 USALAMA NYUMBANI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Kusikiliza kwa Kufasiri**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe katika matini ya kusikiliza,<br>b) kueleza uhusiano kati ya ujumbe wa matini na maisha ya kila siku,<br>c) kujadili mafunzo yanayotokana na ujumbe wa matini,<br>d) kujenga mazoea ya kuhusisha ujumbe katika matini na hali ya maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza masuala yanayozungumziwa katika matini aliyosikiliza kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali,<br>● kusikiliza matini katika vifaa vya kidijitali, kutoka kwa mwalimu au mgeni mwalikwa na kueleza uhusiano wa ujumbe wa matini hiyo na maisha ya kila siku,<br>● kujadili na wenzake mafunzo yanayotokana na ujumbe wa matini,<br>● kushirikiana na mzazi au mlezi kusikiliza na kuchanganua habari katika matini za aina mbalimbali kuhusu suala lengwa. | 1. Ni ujumbe gani uliosikiliza katika matini ambao unafanana na mambo katika jamii yako?<br>2. Unajifunza nini kutokana na ujumbe katika matini ulizosikiliza? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji kutoa hoja na anapoeleza kikamilifu masuala yanayozungumziwa katika habari aliyosikiliza.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza habari.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapohusisha habari inayozungumziwa katika matini aliyosikiliza na maisha ya kila siku katika kutatua matatizo ya jamii.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwaelezea wenzake masuala yanayozungumziwa katika matini aliyosikiliza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojadili na mzazi au mlezi wake kuhusu habari katika matini aliyosikiliza.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji na kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposikiliza matini kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa kufasiri katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama nyumbani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Kina** *Tamthilia*<br>• *Maudhui*<br>• *Dhamira*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya maudhui na dhamira katika fasihi ili kuipambanua,<br>b) kutambua maudhui na dhamira katika tamthilia,<br>c) kujadili maudhui na dhamira katika tamthilia,<br>d) kujenga mazoea ya usomaji wa kazi za kifasihi ili kujenga misingi ya uchambuzi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya maudhui katika fasihi<br>● kutambua maudhui mbalimbali katika tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kujadili na wenzake maudhui ya tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu maudhui,<br>● kuandika maelezo mafupi kuhusu maudhui katika tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kueleza maana ya dhamira katika fasihi,<br>● kutambua dhamira ya tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kujadili na wenzake dhamira katika tamthilia,<br>● kuandika maelezo mafupi kuhusu dhamira ya tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kuwawasilishia mzazi, mlezi au mwenzake uchambuzi wake kuhusu | Je, ni mambo gani muhimu yaliyo katika tamthilia ulizosoma? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | maudhui na dhamira ili wautolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua na kujadili dhamira na maudhui katika tamthilia.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake ufupisho wa dhamira na maudhui ili waujadili na kutolea maoni.
- Uwazaji kina: mwanafunzi anapochanganua maudhui na dhamira katika tamthilia na kuwasilishia wenzake.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake wanapotambua na kujadili dhamira na maudhui katika tamthilia.
- Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kuhusu uwasilishaji wa wengine ili kuwarekebisha na kuwahimiza.
- Umoja: mwanafunzi anapotagusana na wengine ili kutambua na kujadili dhamira na maudhui katika tamthilia.

**Masuala mtambuko:**

Masuala mtambuko anuwai: mwanafunzi anaposoma tamthilia.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maudhui na dhamira katika tamthilia katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama nyumbani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Insha ya mdokezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya insha ya mdokezo ili kuipambanua,<br>b) kubainisha aina za insha ya mdokezo,<br>c) kujadili vipengele vya insha ya mdokezo,<br>d) kuandika insha ya mdokezo kwa kuzingatia vipengele vya uandishi husika,<br>e) kufurahia kuandika insha za mdokezo ili kukuza ubunifu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua maana ya insha ya mdokezo,<br>● kujadili vipengele vya insha ya mdokezo atakachosimulia kutokana na mdokezo kwenye matini au kwenye kikundi,<br>● kubainisha aina za insha ya mdokezo *(kuanzia na kumalizia)* kwa kujadiliana na wenzake,<br>● kusoma kielelezo cha insha kutoka kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>● kueleza vipengele vilivyozingatiwa katika uandishi wa insha ya mdokezo aliyosoma,<br>● kuandika insha ya mdokezo kwa kuzingatia vipengele vya uandishi wa insha za mdokezo,<br>● kuwasilisha insha yake darasani ili wenzake waitolee maoni,<br>● kuwasilishia mzazi au mlezi insha aliyoiandika ili aitolee maoni. | Je, ni vigezo vipi vinavyotumika katika kuandika insha za mdokezo? |

DRAFT

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji na kujadiliana kuhusu insha za mdokezo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma vielelezo vya insha ya mdokezo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya mdokezo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika insha ya mdokezo kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya mdokezo katika katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama nyumbani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Vivumishi**<br><br>• *Vivumishi vya Sifa*<br>• *Vivumishi Viashiria*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vivumishi vya sifa na viashiria/vionyeshi katika matini,<br>b) kutumia vivumishi vya sifa na viashiria/vionyeshi ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi ya vivumishi vya sifa na viashiria katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vivumishi vya sifa na viashiria kwenye chati, kadi maneno au kapu maneno,<br>● kutenga vivumishi vya sifa na viashiria katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwa kuvipigia mstari au kuvikolezea wino katika matini za kidijitali,<br>● kumtajia mwenzake vivumishi vya sifa na viashiria katika mazingira ya shuleni na ya nyumbani,<br>● kutafiti mtandaoni kuhusu vivumishi vya sifa na viashiria,<br>● kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia vivumishi vya sifa na viashiria/vionyeshi ipasavyo,<br>● kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia vivumishi vya sifa na viashiria akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la usalama nyumbani,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kuhusu vivumishi vya sifa na viashiria | Je, kuna tofauti gani kati ya vivumishi vya sifa na vivumishi viashiria? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | alivyotafiti mtandaoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutafiti kuhusu vivumishi vya sifa na viashiria.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vivumishi vya sifa na viashiria.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vivumishi vya sifa na viashiria na kuzitungia sentensi na vifungu sahihi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu vivumishi vya sifa na viashiria.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia vivumishi vya sifa na viashiria.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi vya sifa na viashiria/vionyeshi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama nyumbani na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture.

## 7.0 KUHUDUMIA WENYE MAHITAJI MAALUM

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Usikilizaji Husishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya usikilizaji husishi ili kuubainisha,<br>b) kujadili vipengele vya kuzingatia katik a usikilizaji husishi,<br>c) kufanya mazungumzo yanayozingatia vipengele vya usikilizaji husishi,<br>d) kuchangamkia kushiriki katika usikilizaji husishi ili kujenga uhusiano mwema na wengine. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya usikilizaji husishi akishirikiana na wenzake,<br>● kujadili vipengele vya kuzingatia katika usikilizaji husishi,<br>● kusikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa kutoka kwenye vifaa vya kidijitali akizingatia na kutambua vipengele vya usikilizaji husishi vilivyozingatiwa,<br>● kumsikiliza mwenzake, mwalimu au mgeni mwalikwa akisema kauli au akisoma vifungu vifupi kuhusu suala lengwa na kufasiri hisia zake,<br>● kuigiza kikao cha utoaji nasaha akishirikiana na wenzake huku akizingatia vipengele vya usikilizaji husishi,<br>● kushiriki mazungumzo kuhusu suala lengwa na mzazi, mlezi au mwenzake huku akizingatia | Unaposhiriki katika usikilizaji husishi, utazingatia nini ili kufanikisha usikilizaji? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vipengele vya usikilizaji husishi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili kuhusu vipengele vya kuzingatia katika usikilizaji husishi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia mazungumzo kuhusu suala lengwa.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofasiri hisia za msemaji.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo kuhusu suala lengwa na mzazi au mlezi wake na kujifunza zaidi vipengele vya usikilizaji husishi.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji. Pia mwanafunzi anapoheshimu zamu ya wenzake katika mazungumzo.
- Upendo: mwanafunzi anapowasikiliza wasemaji kwa makini na kujihusisha na hisia zao.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**
Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo akizingatia suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha usikilizaji husishi katika somo la Kiswahili na usikilizaji huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuhudumia wenye mahitaji maalum na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7 .2.1 Ufupisho**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ufupisho ili kuupambanua,<br>b) kujadili vipengele vya ufupisho wa kifungu,<br>c) kufupisha kifungu akizingatia vipengele vya ufupisho,<br>d) kujenga mazoea ya kuwasiliana kwa maelezo mafupi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya ufupisho akishirikiana na wenzake,<br>• kujadili vipengele vya ufupisho wa kifungu akiwa na wenzake,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kutambua kwenye matini andishi au ya kidijitali habari za kimsingi katika makala na kuzieleza kwa usahihi kwa kuzingatia mtazamo wa matini katika matini ya kufupishwa,<br>• kueleza kwa maneno yake habari muhimu katika kifungu alichosoma,<br>• kufupisha kifungu alichosoma kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa habari sahihi kutokana na matini akishirikiana na wenzake,<br>• kuwawasilishia wenzake kazi yake ili waitolee maoni,<br>• kumweleza mzazi au mlezi namna ya kufupisha kifungu kwa kuzingatia | Unazingatia nini unapofupisha kifungu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mpangilio ufaao wa habari sahihi kutokana na matini. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana habari kuu za aya kwenye kifungu alichosoma.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoandaa ufupisho na kuwawasilishia wenzake ili wautolee maoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika ufupisho kwa kuzingatia mpangilio ufaao.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposoma kifungu mtandaoni na kudondoa hoja muhimu.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake wanapojadili vipengele vya ufupisho wa kifungu.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji. Pia, anapojitolea kuiandaa kazi yake ili kuwawasilishia wenzake.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili maneno na hoja muhimu katika kifungu.

**Masuala mtambuko:**

- Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.
- Uongozi na utawala mwema: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa hasa kuhusu maongozi yanayojali watu wote.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufupisho katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuhudumia wenye mahitaji maalum na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Insha ya maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua tamathali mbalimbali za lugha katika insha ya maelezo,<br>b) kueleza jinsi tamathali mbalimbali za lugha zinavyochangia kujenga picha dhahiri katika insha ya maelezo,<br>c) kuandika insha ya maelezo akitumia tamathali mbalimbali za lugha ili kujenga picha dhahiri,<br>d) kufurahia kuandika insha za maelezo akitumia tamathali mbalimbali za lugha ili kujenga picha dhahiri. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua tamathali mbalimbali za lugha katika vielelezo vya insha za maelezo *(k.v. tashbihi, sitiari, uhaishaji na tanakali sauti),*<br>• kutambua jinsi tamathali za lugha katika kielelezo cha insha ya maelezo zinavyochangia kujenga picha dhahiri ya kinachoelezewa akishirikiana na wenzake,<br>• kupigia mstari tamathali mbalimbali zilizotumiwa kwenye kifungu na kutoa maelezo katika kitabu au kifaa cha kidijitali akishirikiana na wenzake,<br>• kuandika insha ya maelezo akitumia tamathali mbalimbali za lugha ili kujenga picha dhahiri katika insha ya maelezo,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni. | Je, unatumia lugha ya aina gani wakati unapotaka kumweleza mtu kitu ili aweze kupata picha kamili? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuandika insha ya maelezo.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha inayosawiri picha halisi ya kitu anachoelezea.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Haki na majuku ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.<br>• Uongozi na utawala mwema: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa hasa kuhusu maongozi yanayojali watu wote. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuhudumia wenye mahitaji maalum na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Vivumishi**<br><br>• *Vivumishi Vimilikishi*<br>• *Vivumishi vya Idadi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vivumishi vimilikishi na vya idadi katika matini,<br>b) kutumia vivumishi vimilikishi na vya idadi ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia matumizi ya vivumishi vimilikishi na vya idadi katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vivumishi vimilikishi, na vya idadi kwenye chati, kadi maneno au kapu maneno akishirikiana na wenzake,<br>• kutenga vivumishi vimilikishi na vya idadi katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino katika matini za kidijitali au za kimaandishi,<br>• kumtajia mwenzake vivumishi vimilikishi na vya idadi katika mazingira ya shuleni,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia vivumishi vimilikishi na vya idadi ipasavyo,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia vivumishi vimilikishi na vya idadi akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la kuhudumia wenye mahitaji maalum,<br>• kumtajia mzazi au mlezi sentensi zenye vivumishi vimilikishi na vya idadi katika mazingira ya nyumbani. | Je, kuna tofauti gani kati ya vivumishi vimilikishi na vya idadi? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia shughuli za ujifunzaji na kuchambua aina mbalimbali za vivumishi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutafiti kuhusu vivumishi lengwa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia vivumishi vya idadi na vimilikishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vivumishi vya idadi na vimilikishi na kuzitungia sentensi na vifungu sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia vivumishi vya idadi na vimilikishi.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vivumishi vimilikishi na vya idadi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuhudumia wenye mahitaji maalum na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

DRAFT

## 8.0 UHALIFU WA MTANDAONI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na kuzungumza** | **8.1.1 Uzungumzaji wa Papo kwa Hapo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya uzungumzaji wa papo kwa hapo ili kuupambanua,<br>b) kutambua vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji wa papo kwa hapo,<br>c) kutoa uzungumzaji wa papo kwa hapo kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uzungumzaji,<br>d) kuchangamkia kutoa uzungumzaji wa papo kwa hapo ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya mazungumzo ya papo kwa hapo akishirikiana na wenzake,<br>• kubainisha vipengele vya kuzingatia katika uzungumzaji wa papo kwa hapo,<br>• kusikiliza uzungumzaji wa papo kwa hapo kuhusu suala lengwa yakitolewa na mwalimu, wenzake, mgeni mwalimu au kutoka kwenye vifaa vya kidijitali na kutathmini vipengele vya uwasilishaji vilivyotumika,<br>• kushiriki katika uzungumzaji wa papo kwa hapo akizingatia vipengele vifaavyo,<br>• kubuni uzungumzaji mwepesi wa papo kwa hapo kuhusu suala lengwa akizingatia vipengele vifaavyo na kuwawasilishia wenzake ili wautathmini. | Unazingatia mambo gani ili kufanikisha uzungumzaji wa papo kwa hapo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojieleza kwa njia wazi katika uwasilishaji wa uzungumzaji wa papo kwa hapo.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga uzungumzaji wa papo kwa hapo kuhusu suala lengwa.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutoa uzungumzaji wa papo kwa hapo kuhusu suala lengwa.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki uzungumzaji wa papo kwa hapo na kujifunza zaidi kuhusu uzungumzaji wa papo kwa hapo. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapoihusisha hadhira katika uzungumzaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake na kutoa mchango katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhiriki na wengine katika uzungumzaji wa papo kwa hapo kuhusu suala lengwa kwa utulivu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Masuala ya usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposhiriki katika uzungumzaji wa papo kwa hapo kuhusu suala lengwa.<br>• Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anaposhiriki katika uzungumzaji wa papo kwa hapo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uzungumzaji wa papo kwa hapo katika somo la Kiswahili na uzungumzaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la uhalifu wa mitandaoni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

DRAFT

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8 .2.1 Kusoma kwa Kina**<br>*Tamthilia*<br>• *Mandhari*<br>• *Ploti*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mandhari na ploti katika tamthilia,<br>b) kueleza umuhimu wa mandhari na ploti ili kuubanisha,<br>c) kujadili mandhari na ploti ya tamthilia aliyosoma,<br>d) kuchangamkia nafasi ya mandhari na ploti katika tamthilia. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua mandhari mbalimbali katika tamthilia akishirikiana na wenzake,<br>• kueleza umuhimu wa mandhari katika katika tamthilia akishirikiana na wenzake,<br>• kuandika kwa ufupi kuhusu mandhari katika tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu mandhari,<br>• kusoma chapisho la tamthilia au kutoka mtandaoni na kutambua mandhari yake,<br>• kutambua ploti ya tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu au kwa kushirikiana na wenzake,<br>• kujadili umuhimu wa ploti ya tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu au na wenzake,<br>• kuandaa muhtasari kuhusu ploti ya tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu ploti ya tamthilia aliyosoma, | 1. Ni mandhari gani unayokumbuka yaliyo katika tamthilia ulizowahi kusoma?<br>2. Ploti ina umuhimu gani katika tamthilia ulizowahi kusoma? |

<table>
<tr><td></td><td></td><td></td><td>• kumweleza mzazi au mlezi kuhusu mandhari na ploti katika tamthilia aliyosoma.</td><td></td></tr>
<tr><td colspan="5">Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili na kuchambua mandhari na ploti katika tamthilia.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha kazi yake darasani.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapochanganua habari katika tamthilia ili kupata mandhari na ploti.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapoeleza au kujadili umuhimu wa mandhari na ploti katika tamthilia.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti muhtasari wa mandhari na ploti.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Maadili:<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake wanapotambua na kujadili mandhari na ploti kwenye tamthilia.<br>• Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kuhusu uwasilishaji wa wengine ili kuwarekebisha na kuwahimiza.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anaposoma na kuchanganua tamthilia.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine ili kutambua na kujadili mandhari na ploti kwenye tamthilia.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Masuala mtambuko:<br>Masuala mtambuko anuwai: mwanafunzi anaposoma tamthilia na kutambua mandhari na ploti.</td></tr>
<tr><td colspan="5">Uhusiano na masomo mengine:<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mandhari na ploti katika tamthilia katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la uhalifu wa mitandaoni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.</td></tr>
</table>

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
| --- | --- | --- | --- | --- |
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Viakifishi**<br><br>• *Alama za Mtajo*<br>• *mshazari*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya alama za mtajo na mshazari katika matini,<br>b) kutumia alama za mtajo na mshazari ipasavyo katika matini,<br>c) kufurahia matumizi yafaayo ya alama za mtajo na mshazari katika matini. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua matumizi ya alama za mtajo na mshazari kwenye matini andishi au za kidijitali,<br>• kuandika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kwa kutumia alama za mtajo na mshazari ipasavyo,<br>• kuandika kwenye kifaa cha kidijitali kifungu kifupi kuhusu suala lengwa akitumia alama za mtajo na mshazari ipasavyo na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili wakitolee maoni,<br>• kushirikiana na wenzake kusahihisha kifungu ambacho hakijatumia alama za mtajo na mshazari ipasavyo,<br>• kuwasomea wenzake kifungu alichoandika na kuwataka waandike maneno, sentensi au vifungu vinavyostahili kuwa na alama za mtajo na mshazari,<br>• kushirikiana na mzazi au mlezi kutafiti mtandaoni au kwenye vitabu | 1. Je, alama za mtajo hutumiwa vipi katika maandishi?<br>2. Je, alama ya mshazari hutumiwa vipi katika maandishi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vya ziada kuhusu matumizi ya alama za mtajo na mshazari. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika kifungu na kuwasambazia wenzake mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya alama za mtajo na mshazari.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kutafiti kuhusu matumizi ya alama za mtajo na mshazari.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Masuala ya usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoandika sentensi na vifungu kuhusu suala lengwa.
- Usalama wa watoto: mwanafunzi anapoandika sentensi na vifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya mtajo na mshazari katika somo la Kiswahili na matumizi hayo katika English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la uhalifu wa mitandaoni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br><br>• *Ngeli ya I-ZI*<br>• *Ngeli ya I-I*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli I-ZI na I-I katika sentensi,<br>b) kutambua nomino za ngeli ya I-ZI na I-I katika matini,<br>c) kutumia nomino za ngeli I-ZI na I-I katika matini kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya I-ZI na I-I ipasavyo katika sentensi na vifungu ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya I-ZI na I-I katika sentensi na mafungu ya maneno,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya I-ZI na I-I,<br>• kuchopoa nomino za ngeli I-ZI na I-I kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au katika tarakilishi,<br>• kutaja majina ya vitu katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya I-ZI na I-I,<br>• kutenga nomino za ngeli ya I-ZI na I-I katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kutunga sentensi au vifungu vyenye upatanisho ufaao wa kisarufi kwa kutumia nomino za ngeli ya I-ZI na I-I akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la uhalifu | 1. Ni vitu gani katika mazingira yako vyenye majina yaliyo katika ngeli ya I-ZI?<br>2. Ni majina yapi unayojua ya ngeli ya I-I? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wa mtandaoni,<br>• kutunga sentensi zenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya I-ZI na I-I akitumia nomino za vitu vilivyo katika mazingira ya nyumbani, na kumsomea mzazi au mlezi wake ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua nomino katika ngeli ya I-ZI na I-I.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi au vifungu akizingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya I-ZI na I-I.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuunda sentensi au vifungu kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya I-ZI na I-I.
  Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizounda kwa kutumia nomino za ngeli ya I-ZI na I-I katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Masuala ya usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za ngeli ya I-ZI na I-I.

DRAFT

| |
|---|
| • Usalama wa watoto: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za ngeli ya I-ZI na I-I. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ngeli na upatanisho wa sarufi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la uhalifu wa mitandaoni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

DRAFT

## 9.0 MAJUKUMU YA MNUNUZI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>• *Sauti /**ch**/*<br>• *Sauti /**sh**/*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti /**ch/** na /**sh**/katika silabi na maneno,<br>b) kutamka sauti /**ch**/ na /sh/ipasavyo katika silabi na maneno,<br>c) kutumia maneno yenye sauti /**ch**/ na /sh/ipasavyo katika matini ili kuyatofautisha kimatamshi,<br>d) kuchangamkia matamshi bora ya sauti **/ch/** na **/sh/**katika mazungumzo ya kawaida ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti /**ch**/ na /**sh**/katika maneno na silabi akishirikiana na wenzake,<br>• kutambua maneno yenye sauti /**ch/** na **/gh/** katika matini andishi au za kidijitali na kuyatamka ipasavyo,<br>• kutunga vitanzandimi vyenye maana akitumia sauti /**ch**/ na /**sh**/na kujirekodi kwa kutumia kifaa cha kidijitali,<br>• kusikiliza na wenzake vitanzandimi alivyovirekodi ili kuvitathmini,<br>• kumwasilishia mzazi au mlezi mazungumzo kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /**ch**/ na /**sh**/**.** | Ni maneno yapi unayoyajua yaliyo na sauti /ch/ na /sh/? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za kutafuta maneno yenye sauti **/ch/** na **/sh/** katika matini.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza vitanza ndimi vyenye sauti /ch/ na /sh/.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotambua na kutofautisha matamshi kuhusu sauti lengwa na pia anapotunga sentensi.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti **/ch/** na **/sh/**na anapochangia katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na mzazi au mlezi kwa kuhusisha matamshi bora ya sauti /ch/ na /sh/**.** |
| **Maadili:**<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wengine nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji na kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kwa heshima na utulivu katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Amani: mwanafunzi anapofanya kazi na wenzake bila migogoro yoyote. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotagusana na maneno ya sauti husika ambayo yanahusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matamshi ya sauti katika somo la Kiswahili na matamshi katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya mnunuzi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Kushawishi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua habari mahususi katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi,<br>b) kutabiri matukio katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi,<br>c) kueleza maana ya msamiati na vifungu vya maneno katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi,<br>d) kujadili ushawishi katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi,<br>e) kuchangamkia usomaji wa ufahamu shawishi ili kukuza hamu ya ujifunzaji. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma ufahamu wa kifungu cha kushawishi kutoka kwa vitabu au vifaa vya kidijitali na kudondoa habari mahususi *(k.v. nani, nini, wapi, lini),*<br>• kutabiri matukio katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi akishirikiana na wenzake,<br>• kueleza maana ya msamiati kuhusu suala lengwa (*k.v. maneno na nahau*) katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi na kuueleza kwa kutumia kamusi akishirikiana na wenzake,<br>• kujadili ushawishi katika kifungu cha ufahamu akishirikiana na wenzake,<br>• kuwawasilishia wenzake kazi yake ili wamtolee maoni. | Ni kwa njia gani tunaweza kutambua ujumbe wenye lengo la kushawishi katika habari? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili ushawishi katika kifungu cha ufahamu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposakura mtandaoni ili kupata matini mbalimbali na kuzisoma na kudondoa habari

| |
|---|
| mahususi.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotabiri matukio katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kwa uwajibikaji na kuzingatia maadili.<br>• Umoja: mwanafunzi anapotagusana na wenzake ili kujadili ushawishi katika kifungu cha ufahamu. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposoma ufahamu kuhusu suala lengwa.<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposoma ufahamu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha usomaji wa kifungu cha kushawishi katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya mnunuzi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Insha ya masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vinavyozingatiwa kujenga wazo katika insha ya masimulizi,<br>b) kujadili vipengele vinavyojenga wazo katika aya kuhusu insha ya masimulizi,<br>c) kuandika insha ya masimulizi akikuza wazo katika aya ipasavyo,<br>d) kufurahia utunzi wa insha za masimulizi zenye mpangilio mzuri wa wazo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vinavyozingatiwa kujenga wazo (*k.v. mada, utangulizi, kati, hitimisho)* katika insha ya masimulizi katika matini za kimaandishi na za kidijitali,<br>• kutambua ukuzaji wa wazo katika kila aya ya insha ya masimulizi katika matini za kimaandishi au za kidijitali,<br>• kueleza jinsi wazo lilivyokuzwa katika kila aya ya insha ya masimulizi *(k.v. kila wazo kuu kuwa katika aya yake, kutoa maelezo toshelevu kwa kila hoja kuu katika aya yake, kuepuka urudiaji au uchanganyaji wa hoja katika aya),*<br>• kushirikiana na wenzake kujadili vipengele vinavyojenga mawazo,<br>• kuandika vidokezo vya insha vinavyozingatia ukuzaji wa wazo katika kila aya,<br>• kuandika insha ya masimulizi akizingatia ukuzaji wa wazo katika kila aya na vipengele vinavyojenga | Je, unawezaje kulikuza wazo vizuri katika insha ya masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mawazo hayo,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni,<br>• kushirikiana na wenzake kusahihisha insha ya maelezo aliyoandika kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia ukuzaji wa wazo katika kila aya. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa insha ya masimulizi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapolikuza wazo katika kila aya katika utungo wake kwa ufasaha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika na kuwasomea wenzake insha.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.
- Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.

DRAFT

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi katika somo la English
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya mnunuzi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br><br>• *Ngeli ya U-U*<br>• *Ngeli ya U-YA*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-U na U-YA katika sentensi,<br>b) kutambua nomino za ngeli ya ya U-U na U-YA katika matini,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya U-U na U-YA katika matini kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino katika ngeli ya U-U na U-YA ipasavyo ili kuimarisha umilisi wa lugha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya U-U na U-YA katika sentensi na vifungu vya maneno,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-U na U-YA,<br>• kuchopoa nomino za ngeli ya U-U na U-YA kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au katika tarakilishi,<br>• kutaja majina ya vitu katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya U-U na U-YA,<br>• kutenga nomino za ngeli ya U-U na U-YA katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi | 1. Ni vitu gani katika mazingira yako vyenye majina yaliyo katika ngeli ya U-U?<br>2. Ni vitu gani katika mazingira yako vyenye majina yaliyo katika ngeli ya U-YA? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vyenye upatanisho ufaao wa ngeli ya U-U na U-YA akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la majukumu ya mnunuzi,<br>• kuwasilisha kazi yake darasani au kuwasambazia wenzake mtandaoni ili waitolee maoni,<br>• kutunga sentensi zenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya U-U na U-YA akitumia nomino za vitu vilivyo katika mazingira ya nyumbani, na kumsomea mzazi au mlezi wake ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi au vifungu vifupi akizingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya U-U na U-YA.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuunda sentensi au vifungu vifupi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa U-U na U -YA.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizounda kwa kutumia nomino za ngeli ya U-U na U-YA katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.

DRAFT

| |
|---|
| • Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za ngeli ya U-U na U- YA.<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ngeli na upatanisho wa kisarufi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya mnunuzi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies. |

DRAFT

## 10.0 KUKABILIANA NA HISIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Hadithi**<br><br>• *Hurafa*<br>• *Hekaya*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hurafa na hekaya ili kuzibainisha,<br>b) kueleza ujumbe katika hurafa na hekaya,<br>c) kujadili vipengele vya uwasilishaji wa hurafa na hekaya,<br>d) kusimulia hurafa na hekaya kwa kuzingatia vipengele vya uwasilishaji,<br>e) kufurahia hurafa na hekaya kama vipera vya fasihi simulizi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza kielelezo cha hadithi ya hurafa na hekaya kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>● kueleza maana ya hurafa na hekaya ili kuzibainisha akishirikiana na wenzake,<br>● kueleza ujumbe katika hurafa na hekaya,<br>● kujadili na mwenzake vipengele vya uwasilishaji wa hurafa na hekaya,<br>● kuwasilisha hurafa na hekaya kwa kuzingatia vipengele vya uwasilishaji *(kiini cha hadithi, kiwango cha lugha, mpangilio wa matukio, sauti, ishara za mwili),*<br>● kujirekodi akitamba hurafa na hekaya kwa kutumia vifaa vya kidijitali na kusikiliza,<br>● kushirikiana na mzazi au mlezi kutambua hurafa na hekaya kutoka kwa jamii yake na kujadili ujumbe | 1. Je, hadithi ambayo umewahi kusikiliza ilihusu wanyama gani?<br>2. Je, hurafa na hekaya hutofautianaje? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | unaojitokeza katika hadithi hizo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposimulia hurafa na hekaya na kuwashirikisha wenzake katika masimulizi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia hurafa na hekaya.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposimulia hurafa na hekaya kwa wenzake kwa kuzingatia vipengele vya kimsingi vya uwasilishaji.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha hurafa na hekaya ipasavyo kwa wenzake.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposimulia hurafa na hekaya akiwa na mzazi au mlezi wake na kuchangamkia kutafiti zaidi kuhusu hadithi za masimulizi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anaposimulia hadithi kuhusu suala lengwa uonoulimwengu wake unakua.
- Masuala ya afya ya akili: mwanafunzi anaposimulia hadithi kuhusu suala lengwa uonoulimwengu wake unakua.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uwasilishaji wa hurafa na hekaya katika somo la Kiswahili na uwasilishaji huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kukabiliana na hisia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>*Wahusika katika tamthilia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua wahusika katika tamthilia aliyosoma,<br>b) kujadili sifa za wahusika katika tamthilia,<br>c) kujadili mafunzo yanayotokana na wahusika katika tamthilia,<br>d) kujenga mazoea ya usomaji wa kazi za kifasihi ili kukuza hamu ya ujifunzaji. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua wahusika katika tamthilia aliyoisoma,<br>● kujadili na wenzake sifa za wahusika katika tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kuigiza wahusika katika tamthilia akiwa na wenzake ili kukuza uelewa wa sifa zao,<br>● kueleza uhusiano kati ya wahusika katika tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kutazama video kuhusu wahusika katika tamthilia aliyosoma,<br>● kuandaa muhtasari kuhusu sifa za wahusika katika video aliyotazama,<br>● kujadili mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika akishirikiana na wenzake. | 1. Ni mambo yapi yanayokuelekeza kuwaelewa wahusika katika tamthilia?<br>2. Je, ni mambo gani tunayoweza kujifunza kutokana na wahusika wa tamthilia? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili sifa za wahusika.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza na wenzake wahusika katika tamthilia. | | | | |

| |
|---|
| ● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotazama video kuhusu wahusika katika tamthili.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza wahusika katika tamthilia.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua sifa za wahusika katika tamthilia. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapochambua tamthilia.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua majukumu mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anaposoma tamthilia yenye uonoulimwengu wake unakua kutokana na maudhui yaliyomo.<br>• Masuala mtambuko anuwai: mwanafunzi anaposoma tamthilia. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya wahusika katika tamthilia na dhana hiyo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kukabiliana na hisia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Barua ya Kuomba Msaada**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kimuundo vya barua rasmi ya kuomba msaada,<br>b) kutambua ujumbe katika barua rasmi ya kuomba msaada,<br>c) kuandika barua rasmi ya kuomba msaada kwa kuzingatia ujumbe, muundo na lugha ifaayo,<br>d) kufurahia kujieleza ifaavyo kwa njia ya barua. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kujadili vipengele vya kimuundo vya barua rasmi ya kuomba msaada,<br>● kutambua ujumbe unaoafiki barua rasmi ya kuomba msaada,<br>● kujadili na wenzake kuhusu lugha inayofaa katika uandishi wa barua rasmi ya kuomba msaada,<br>● kuandika barua rasmi ya kuomba msaada kuhusu masuala mbalimbali na kuwasomea wenzake darasani ili waitolee maoni,<br>● kuandika barua ya kuomba msaada katika kifaa cha kidijitali na kuwasambazia wenzake kupitia mtandao ili waitolee maoni. | 1. Je ni mambo gani yanayoweza kukufanya kuomba msaada?<br>2. Je, ni vipengele vipi unazingatia wakati unapoandika barua ya kuomba msaada? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kutoa mchango wake.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika barua na kuisambaza kwa mtandao. | | | | |

- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika barua rasmi ya kuomba msaada.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**
- Mtazamo wa ukuaji wa binadamu: mwanafunzi anaopandika barua ya kuomba msaada kuhusu suala lengwa.
- Masuala ya afya ya akili: mwanafunzi anaopandika barua ya kuomba msaada kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa barua ya kuomba msaada katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kukabiliana na hisia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Vitenzi na Vielezi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kinyume ili kuibainisha,<br>b) kutambua vinyume vya vitenzi na vielezi katika matini,<br>c) kutumia vinyume vya vitenzi na vielezi ipasavyo katika matini,<br>d) kuchangamkia kutumia vinyume vya vitenzi na vielezi katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kujadili maana ya kinyume akiwa na mwenzake,<br>● kutambua vinyume vya vitenzi *na* vielezi kwa kutumia kadi maneno, mti maneno, kapu maneno,<br>● kutambua vinyume vya vitenzi na vielezi katika matini *(k.v. orodha ya maneno, sentensi na vifungu vya maneno),*<br>● kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya vinyume vya vitenzi na vielezi kutoka kwa sentensi mbalimbali kwenye vitabu, tarakilishi au chati,<br>● kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia vinyume vya vitenzi na vielezi ipasavyo,<br>● kutunga sentensi au vifungu vifupi akitumia vinyume vya vitenzi na vielezi ipasavyo akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la kukabiliana na | 1. Je, ni vinyume gani vya vitenzi unavyojua?<br>2. Je, unajua vinyume gani vya vielezi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | hisia,<br>● kusakura mtandaoni au kutafiti katika vitabu vya ziada ili kupata vinyume zaidi vya vitenzi na vielezi,<br>● kumsomea mzazi au mlezi sentensi alizotunga kuhusu vinyume vya vitenzi na vielezi. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutambua vinyume vya vitenzi na vielezi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vinyume vya vitenzi na vielezi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha vinyume vya vitenzi na vielezi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua vinyume vya vitenzi na vielezi na kuvitungia sentensi sahihi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi/mlezi wake sentensi alizotunga kuonyesha vinyume vya vitenzi.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**
- Masuala ya afya ya akili: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume vya vitenzi na vielezi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kukabiliana na hisia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

## 11.0 HAKI ZA WATOTO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **11.1.1 Kuzungumza kwa Kutumia Vidokezo vya Hoja**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua umuhimu wa kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja,<br>b) kutambua miktadha katika jamii ambapo kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja hufanywa,<br>c) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja,<br>d) kutoa mazungumzo kwa kutumia vidokezo ifaavyo,<br>e) kujenga mazoea ya kutumia vidokezo katika mazungumzo ili | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja,<br>● kujadili na wenzake umuhimu wa kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja,<br>● kutambua miktadha katika jamii yake ambamo anahitaji kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja,<br>● kujadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja,<br>● kusikiliza au kutazama aina mbalimbali za mazungumzo kutoka kwenye vifaa vya kidijitali, mgeni mwalikwa au wenzake na kubainisha vipengele vilivyozingatiwa,<br>● kuandaa vidokezo kuhusu suala lengwa,<br>● kuwawasilishia wenzake mazungumzo kuhusu suala lengwa kwa kutumia vidokezo alivyoandaa | Kwa nini ni muhimu kuandaa vidokezo unapozungumza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kufanikisha mawasiliano. | ili wayatolee maoni,<br>● kumwasilishia mzazi au mlezi vidokezo vya mazungumzo kuhusu suala lengwa ili atoe maoni yake. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuwasilisha mazungumzo kuhusu suala lengwa
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandaa vidokezo kuhusu suala lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake mazungumzo kuhusu suala lengwa.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposikiliza au kutazama aina mbalimbali za mazungumzo na kubainisha vipengele vilivyozingatiwa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake zamu ya kushiriki katika mazungumzo bila kuwakata kauli.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali alivyotumia kujifunzia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wengine na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Haki za watoto: mwanafunzi anapozungumza kuhusu suala lengwa.
- Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anapozungumza kuhusu suala lengwa na kurelea haki ya usalama.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **11.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kuteua matini ifaayo ya kujisomea,<br>b) kueleza ujumbe katika matini ya kujichagulia,<br>c) kutambua maana za msamiati na matumizi mengine ya lugha katika matini ya kujichagulia,<br>d) kujenga mazoea ya kusoma matini mbalimbali katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kuteua matini ifaayo ya kujisomea,<br>● kueleza ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyoisoma,<br>● kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia *(k.v. ya usalama barabarani (mfano;* tabia hatarishi kwa watumiaji wengine wa barabara, kutoa maoni na kuripoti kuhusu tabia hatarishi) *ya kisayansi, ya kisiasa, ya kihistoria, ya kifasihi,),*<br>● kutumia kamusi kutafuta maana za maneno asiyoyajua,<br>● kujenga rekodi ya msamiati aliojifunza katika kitabu,<br>● kutunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma,<br>● kusakura mtandaoni na kujichagulia matini ya ziada kisha aisome. | 1. Unavutiwa zaidi na nini unaposoma makala ya kujichagulia?<br>2. Unazingatia mambo gani wakati wa kusoma makala ya kujichagulia? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kuwasilisha muhtasari wa matini aliyojichagulia na kueleza ujumbe wa makala.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kujichagulia matini ya kusoma. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Haki za watoto: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa.<br>● Utunzi na usalama wa watoto: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa mapana katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.3 Kuandika** | **11.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Insha ya maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya insha ya maelezo,<br>b) kuandika insha ya maelezo ipasavyo kwa kuzingatia vipengele vyake,<br>c) kufurahia kuandika insha za maelezo katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya insha ya maelezo kwa kurejelea matini mbalimbali,<br>● kutafiti maktabani au mtandaoni vipengele vya insha ya maelezo,<br>● kujadili na wenzake vipengele vya insha ya maelezo alivyotafiti mtandaoni,<br>● kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia vipengele vifaavyo,<br>● kuwasomea wenzake insha aliyoandika au kuwasambazia kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni,<br>● kushirikiana na wenzake kusahihisha insha walizoandika na kutoleana maoni kwa amani na upendo. | Je, ni vipengele gani vya kuzingatia katika kuandika insha ya maelezo? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadili vipengele vya insha ya maelezo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha ya maelezo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake kwa ufasaha insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha nzuri na kuwasomea wenzake.

DRAFT

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Haki za watoto: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi**<br><br>• *Kutendeka*<br>• *Kutendewa*<br>• *Kutendatenda*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda katika vitenzi,<br>b) kutumia vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda ipasavyo ili kuimarisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda mtawalia,<br>• kuteua vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda mtawalia, kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>• kutenga vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda katika sentensi na vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari,<br>• kugeuza vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda | Kwa nini ni muhimu kujifunza kauli za vitenzi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ipasavyo,<br>● kutunga sentensi au vifungu vifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la haki za watoto, | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kutoa mchango wake katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vitenzi katika kauli lengwa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia vitenzi katika kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua viambishi vya kauli ya kutendeka, kutendewa na kutendatenda na kuandika
- vitenzi katika kauli hizo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Haki za watoto: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mnyambuliko wa vitenzi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la haki za watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Studies.

DRAFT

## 12.0 MAGONJWA YASIYOAMBUKIZWA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **12.1.1 Kusikiliza kwa Makini**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza habari katika matini ya kusikiliza,<br>b) kukadiria maana ya msamiati mahususi na vifungu katika matini ya kusikiliza,<br>c) kudondoa habari muhimu katika matini aliyosikiliza kwa kufuata mpangilio ufaao,<br>d) kujenga mazoea ya kufurahia kusikiliza vifungu vya kusikiliza ili kuimarisha uwezo wa kusikiliza. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza matini kutoka kifaa cha kidijitali au mwalimu wake,<br>● kutambua hoja muhimu katika habari aliyosikiliza kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, kifaa cha kidijitali, mgeni mwalikwa au wenzake,<br>● kueleza hoja muhimu aliyotambua kutoka matini aliyosikiliza,<br>● kukadiria maana ya msamiati mahususi na vifungu katika matini aliyosikiliza,<br>● kuelezea mwenzake maana ya msamiati katika matini ya kusikiliza,<br>● kudondoa habari muhimu katika matini aliyosikiliza kwa kufuata mpangilio ufaao. | Je, kwa nini ni muhimu kuwa na mpangilio ufaao wa hoja kutoka habari uliyosikiliza? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchangia katika shughuli za ujifunzajina kuwatolea

| |
|---|
| wenzake hoja muhimu.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kusikiliza na kuwatajia wenzake hoja muhimu kuhusu suala lengwa kwa ufupi.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposikiliza habari, kuichanganua na kutambua hoja muhimu na kuziwasilisha kwa mpangilio ufaao.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutafiti kwenye mtandao kuhusu suala lengwa na kuwasilisha hoja kuu kwa mpangilio ufaao.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoiwasilisha upya habari aliyosikiliza kwa mpangilio ufaao wa hoja. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wengine fursa ya kutambua na kupanga hoja muhimu bila kuwakatiza.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposikiliza matini kuhusu suala lengwa.<br>● Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapodondoa habari muhimu kutoka na matini kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa makini katika somo la Kiswahili na katika somo la English<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yasiyoambukizwa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Integrated Science. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.2 Kusoma** | **12.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) Kueleza vipengele vya kusoma kwa ufasaha ili kuvibainisha,<br>b) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>c) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>d) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>e) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>f) kuridhia kusoma makala kwa kuzingatia vipengele vinavyofanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha *(matamshi bora, kasi ifaayo, sauti ifaayo, ishara zifaazo),*<br>● kutazama vielelezo vya video za watu wanaosoma kwa ufasaha makala *(k.v. hotuba, taarifa ya habari),*<br>● kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali akizingatia matamshi bora,<br>● kusoma kifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno sahihi yasiyopungua 105 kwa dakika*),<br>● kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo *(k.v. kiwango cha sauti na kiimbo),*<br>● kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo | Je, unaposoma kifungu unazingatia mambo gani ili kufanikisha usomaji? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | panapofaa *(k.v. ishara za uso na mikono),*<br>● kusoma mbele ya wenzake kazi yake ili wamtolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na kujadiliana na wenzake kuhusu vipengele vya kimsingi vya kusoma kwa ufasaha.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa ufasaha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia ishara wakati wa kusoma kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kusoma anakuza hamu ya ujifunzaji.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzajiwanapojadili vipengele vya usomaji bora.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika mjadala wakati wa shughuli ya ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuwasomea wenzake kifungu.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake kujadili vipengele vya usomaji bora.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.
- Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufasaha katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yasiyoambukizwa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Integrated Science.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.3 Kuandika** | **12.3.1 Insha za Kiuamilifu**<br><br>*Hotuba ya kutoa ufafanuzi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hotuba ya kutoa ufafanuzi,<br>b) kutambua hotuba ya kutoa ufafanuzi katika matini,<br>c) kujadili ujumbe, lugha na muundo wa hotuba ya kutoa ufafanuzi,<br>d) kuandika hotuba ya kutoa ufafanuzi kwa kuzingatia vipengele vyake,<br>e) kuchangamkia nafasi ya hotuba ya kutoa ufafanuzi katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya hotuba ya kutoa ufafanuzi,<br>● kujadiliana na wenzake kuhusu ujumbe (*unaolenga kinachotolewa ufafanuzi),* lugha (*nyepesi inayoeleweka*) na muundo ufaao wa hotuba ya kutoa ufafanuzi,<br>● kujadili na wenzake miktadha inayochochea hotuba ya kutoa ufafanuzi,<br>● kujadili na wenzake vidokezo vinavyoweza kutumiwa katika kuandika hotuba ya kutoa ufafanuzi,<br>● kuandika hotuba ya kutoa ufafanuzi kuhusu suala lengwa akizingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao kisha awasambazie wenzake mtandaoni au kuwasomea darasani ili waitolee maoni,<br>● kuandika hotuba ya kutoa ufafanuzi kuhusu suala linaloathiri jamii yao kisha amsomee mzazi au mlezi ili aitolee maoni. | Ni mambo gani ya kuzingatia katika kutoa hotuba ya ufafanuzi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji kujadili kuhusu vipengele vya kuandika hotuba ya kutoa ufafanuzi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika hotuba ya kutoa ufafanuzi na kusambazia wenzake mtandaoni ili waitolee maoni.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoandika hotuba ya kutoa ufafanuzi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anpomsomea mzazi au mlezi hotuba ya kutoa ufafanuzi. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>● Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapoandika hotuba kuhusu suala lengwa.<br>● Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapoandika hotuba kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa hotuba ya kutoa ufafanuzi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yasiyoambukizwa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Integrated Science. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.4 Sarufi** | **12.4.1 Aina za Sentensi**<br><br>*Sentensi changamano*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya sentensi changamano ili kuipambanua kutambua sentensi changamano katika matini,<br>b) kutumia sentensi changamano ipasavyo katika matini,<br>c) kuonea fahari matumizi ya sentensi changamano katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya sentensi changamano,<br>• kutenga sentensi changamano katika orodha ya sentensi kwenye vitabu, chati au tarakilishi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino,<br>• kubainisha sentensi changamano zinazojitokeza katika,<br>• kutunga sentensi changamano ipasavyo akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la magonjwa yasiyoambukizwa,<br>• kuwawasilishia wenzake darasani sentensi changamano alizotunga ili wazitathmini,<br>• kumtungia mzazi au mlezi sentensi changamano zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani. | Ni nini tofauti kati ya sentensi changamano na aina zingine za sentensi unazozijua? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua sentensi changamano.

DRAFT

| |
|---|
| • Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia sentensi changamano.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua sentensi changamano katika kifungu.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake sentensi changamano zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya afya ya kujikinga: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.<br>• Afya ya mtu binafsi: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya sentensi changamano katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa yasiyoambukizwa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Agriculture na Integrated Science. |

DRAFT

## 13.0 HESHIMA KWA TAMADUNI ZA WENGINE

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **13.1.1 Hadithi**<br><br>*Wahusika*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua wahusika katika hadithi,<br>b) kuchambua sifa za wahusika katika hadithi,<br>c) kueleza mafunzo kutokana na wahusika katika hadithi,<br>d) kufurahia kushiriki katika uchambuzi wa wahusika katika hadithi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua washiriki katika hadithi inayosimuliwa *(k.v. fanani, hadhira)*,<br>● kutambua wahusika katika hadithi inayosimuliwa,<br>● kutambua sifa za wahusika katika hadithi aliyosikiliza kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au vifaa vya kidijitali,<br>● kuchambua wahusika katika hadithi aliyosikiliza,<br>● kueleza mafunzo kutokana na wahusika katika hadithi,<br>● kutamba hadithi akiwa na wenzake huku wakichukua majukumu mbalimbali *(k.v. fanani, hadhira)*,<br>● kutunga hadithi fupi ambayo ina wahusika wanyama kuhusu suala lengwa na kuwawasilishia wenzake darasani ili wachambue wahusika, | Je, hadithi uliyowahi kusimuliwa ilikuwa na wahusika gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuwasilishia mzazi au mlezi uchambuzi wa sifa za wahusika katika hadithi aliyosikiliza. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kuchambua wahusika katika hadithi akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia hadithi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobuni hadithi na kuwawasilishia wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochanganua wahusika na nafasi yao katika hadithi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza nafasi ya mhusika katika hadithi au kusimulia wenzake hadithi kwa ukakamavu.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi kushiriki katika kuchanganua wahusika katika hadithi mbalimbali.
- Masuala mtambuko anuawi: mwanafunzi anapochambua hadithi.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya wahusika katika hadithi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la heshima kwa tamaduni za wengine na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.2 Kusoma** | **13.2.1 Kusoma kwa Kina** *Tamthilia*<br><br>*Mbinu za Lugha*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mbinu za lugha katika tamthilia,<br>b) kueleza umuhimu wa mbinu za lugha zilizotumiwa katika tamthilia,<br>c) kufurahia kuchanganua matumizi ya mbinu za lugha katika fasihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mbinu za lugha kwenye tamthilia,<br>● kueleza umuhimu wa mbinu za lugha zilizotumiwa katika tamthilia iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kuhakiki uwasilishaji wa wenzake kuhusu mbinu za lugha katika tamthilia na kuutolea maoni,<br>● kufanya utafiti maktabani au mtandaoni kuhusu matumizi ya mbinu za lugha katika tamthilia,<br>● kuwasilishia mzazi au mlezi uchambuzi wa matumizi ya mbinu za lugha katika tamthilia aliyosoma. | 1. Tamthilia hutumia mbinu gani za lugha?<br>2. Mbinu za lugha zina umuhimu gani katika tamthilia? |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kutambua na kujadiliana kuhusu mbinu za lugha katika tamthilia aliyosoma.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilishia wenzake muhtasari wa matumizi ya mbinu za lugha katika tamthilia kwa kutetea hoja zake.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti maktabani na mtandaoni kuhusu matumizi ya tamathali za lugha katika tamthilia aliyoisoma.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapodhamini maoni ya wenzake.<br>● Upendo: mwanafunzi anaposhirikiana vizuri na wenzake.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapochukua jukumu la kutafiti kuhusu matumizi ya mbinu za lugha maktabani na mtandaoni.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai: mwanafunzi anaposoma tamthilia. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha mbinu za lugha katika tamthilia na mbinu hizo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la heshima kwa tamaduni za wengine na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.3 Kuandika** | **13.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Insha ya maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya insha ya maelezo kuhusu mahali,<br>b) kujadili vipengele vya insha ya maelezo kuhusu mahali,<br>c) kuandika insha ya maelezo inayodhihirisha sifa za mahali,<br>d) kuonea fahari utoaji wa maelezo kamilifu kuhusu kitu au jambo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vigezo vya kimsingi katika uandishi wa insha ya maelezo,<br>● kujadiliana na wenzake kuhusu mada ya insha ya maelezo,<br>● kujadili na wenzake vipengele vya insha ya maelezo kutokana na kielelezo cha insha,<br>● kuandaa vidokezo vya insha ya maelezo kuhusu mahali panapolengwa katika insha ya maelezo,<br>● kutumia lugha inayojenga picha ya kinachoelezewa,<br>● kuandika insha ya maelezo inayotoa sifa za mahali akizingatia muundo ufaao na inayohusisha suala lengwa kisha awasomee wenzake darasani,<br>● kubuni insha ya maelezo inayotoa sifa za mahali kisha awasambazie wenzake mtandaoni ili waitolee maoni,<br>● kutolea insha za wenzake maoni kwa upendo,<br>● kumsomea mzazi au mlezi insha ya | Je, ni vigezo vipi vinavyotumika katika kuandika insha ya maelezo? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kubuni aliyoandika ili aitolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika insha ya maelezo na kuisambaza kwa mtandao.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapobuni insha ya maelezo na kumsomea mzazi/mlezi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la heshima kwa tamaduni za wengine na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.4 Sarufi** | **13.4.1 Ukanushaji kwa Kuzingatia Hali**<br>• *Hali ya mazoea*<br>• *Hali timilifu*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ukanushaji ili kuupambanua,<br>b) kutambua ukanushaji kwa kuzingatia hali ya mazoea na timilifu katika matini,<br>c) kukanusha sentensi kwa kuzingatia hali ya mazoea na timilifu,<br>d) kuchangamkia kukanusha sentensi katika hali ya mazoea na timilifu ili kukuza mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua hali ya mazoea na timilifu kutoka kwenye chati, mti maneno, vitabu au vifaa vya kidijitali,<br>• kutambua ukanushaji wa sentensi katika hali ya mazoea na timilifu,<br>• kuchagua sentensi zinazoonyesha ukanushaji wa hali ya mazoea na timilifu kutoka kwenye mchanganyiko wa sentensi kutoka kwenye vitabu, tarakilishi au chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia hali ya mazoea na timilifu akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la heshima kwa tamaduni za wengine,<br>• kukanusha sentensi au vifungu alivyotunga kisha awatumie | 1. Je, unapotaka kukanusha sentensi unazingatia nini?<br>2. Je, ukanushaji wa hali ya mazoea na timilifu hutofautianaje? |

DRAFT

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake kupitia vifaa vya kidijitali au kuwasomea darasani ili wazitolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki shughuli za ujifunzaji na kujadiliana kuhusu ukanushaji wa hali ya mazoea na timilifu.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotunga sentensi na kuwasambazia wenzake wazitolee maoni.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapowasambazia wenzake sentensi alizotunga katika mtandao.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha ukanushaji wa sentensi katika hali tofauti.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua ukanushaji wa hali na kuutungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ukanushaji kwa kuzingatia hali katika somo la Kiswahili na ukanushaji huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la heshima kwa tamaduni za wengine na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

DRAFT

## 14.0 KUWEKA AKIBA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **14.1.1 Hadithi**<br><br>*Matumizi ya Lugha*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya lugha vinavyotumika katika hadithi,<br>b) kujadili umuhimu wa vipengele vya lugha vinavyotumika katika hadithi,<br>c) kusimulia hadithi kwa kutumia vipengele vya lugha ipasavyo,<br>d) kuonea fahari uchanganuzi wa lugha katika hadithi kama utungo wa fasihi simulizi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya lugha kwa kusikiliza hadithi kutoka kwa mwalimu au vifaa vya kidijitali,<br>• kujadili umuhimu wa vipengele vya lugha vilivyotumika katika hadithi walizosikiliza,<br>• kusimulia hadithi kwa kutumia vipengele vya lugha,<br>• kuwawasilishia wenzake hadithi aliyotunga ili watambue vipengele vya lugha vilivyotumika,<br>• kushirikiana na mzazi au mlezi kusikiliza hadithi na kutambua vipengele vya lugha vilivyotumika. | 1. Ni mbinu gani za lugha zinazotumika katika masimulizi ya hadithi?<br>2. Matumizi ya lugha katika hadithi yana umuhimu gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasilisha kazi yake kwa wenzake na kushirikiana katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga na kuwatambia wenzake hadithi kwa kuzingatia vipengele vya lugha.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapotambua vipengele vya lugha na kuvitumia katika utambaji wa hadithi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposikiliza hadithi zinazohusu suala lengwa.<br>• Umaskini: mwanafunzi anaposimulia hadithi zinazohusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya lugha katika hadithi ya Kiswahili na matumizi hayo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuweka akiba na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Mathematics. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.2 Kusoma** | **14.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Mjadala*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha mjadala,<br>b) kutambua msamiati mpya katika kifungu cha mjadala,<br>c) kuchambua mitazamo katika kifungu cha mjadala,<br>d) kuridhia kusoma kifungu cha mjadala ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kudondoa habari mahususi *(k.v. nani, nini, wapi, lini)* katika kifungu cha ufahamu cha mjadala,<br>• kutambua msamiati mpya *(k.v. maneno na nahau)* katika kifungu cha ufahamu cha mjadala na kuueleza kwa kutumia kamusi,<br>• kueleza maana ya msamiati uliotumiwa kwenye kifungu cha ufahamu cha mjadala na kutunga sentensi akiutumia,<br>• kuchambua mitazamo iliyo katika kifungu cha ufahamu cha mjadala,<br>• kuwawasilishia wenzake kazi yake ili waitolee maoni. | 1. Utawezaje kutambua habari mahususi katika hadithi unayoisoma?<br>2. Je, unazingatia nini unaposoma vifungu vya ufahamu? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasilisha kazi yake kwa wenzake na kushirikiana katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwawasilishia wenzake kazi yake. | | | | |

| |
|---|
| • Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kusoma kifungu na kujibu maswali.<br>• Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapojadili mitazamo katika kifungu cha mjadala. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapodondoa habari kutokana na ufahamu kuhusu suala lengwa.<br>• Umaskini: mwanafunzi anapochambua ufahamu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha usomaji wa kifungu cha mjadala katika somo la Kiswahili na usomaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuweka akiba na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Mathematics. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.3 Kuandika** | **14.3.1 Insha za Maelekezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kujadili vipengele vya insha ya maelekezo,<br>b) kuandika insha ya maelekezo akizingatia vipengele vyake muhimu,<br>c) kufurahia kuandika insha za maelekezo akizingatia vipengele vyake muhimu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kujadili vipengele vya insha ya maelekezo *(k.v. matumizi ya lugha, mpangilio ufaao wa maelekezo, uangavu, ubanaji),*<br>• kutambua maneno mwafaka, mpangilio mzuri wa sentensi na mpangilio sahihi wa hatua katika kielelezo cha insha ya maelekezo kutoka kwa mwalimu, kwenye maandishi *(k.v. vitabu, chati)* au vifaa vya kidijitali,<br>• kuteua maneno yatakayosaidia kufanikisha maelekezo *(k.v. vielezi vya mahali: kulia, kushoto; vitenzi k.v. pinda, elekea, kata; vielekezi vya kiasi: vijiko viwili, nyanya tatu),*<br>• kuandaa mpangilio ufaao wa sentensi zinazofuatana kulingana na maelekezo anayotaka kutoa *(k.v.* maelekezo ya mahali: *Tembea hadi mwendo wa kilomita moja. Ukifika kwenye zahanati upinde kulia;* | Je, unapoandika insha ya maelekezo unazingatia mambo gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | maelekezo ya mapishi*: weka unga vikombe vitatu kwenye bakuli, tia sukari vijiko vitano vikubwa;* maelekezo ya mtihani: *Jibu maswali matatu, swali la kwanza ni la lazima),*<br>• kushiriki kujadili maneno, sentensi na hatua zinazoafiki maelekezo yaliyolengwa,<br>• kuandika insha ya maelekezo akizingatia uteuzi mwafaka wa maneno, sentensi na hatua ili kumjengea msomaji taswira kamili ya kile kinachoelekezwa,<br>• kuwasomea wenzake insha ya maelekezo aliyoandika au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika insha kwa ufasaha na kuwasomea wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia insha yake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoteua msamiati mwafaka na mpangilio ufaao wa hatua na sentensi sahihi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha aliyoandika.

DRAFT

|  |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>• Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha za maelekezo katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuweka akiba na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Mathematics. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.4 Sarufi** | **14.4.1 Udogo wa Nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika hali ya udogo katika matini,<br>b) kubadilisha nomino za hali ya wastani kuwa katika hali ya udogo,<br>c) kutumia nomino katika hali ya udogo ipasavyo,<br>d) kuonea fahari kutumia nomino katika hali ya udogo katika sentensi. | Mwanafunzi:<br>• kutambua nomino katika hali ya udogo kwenye orodha ya nomino, chati, kadi maneno, kapu maneno, sentensi, vifungu vya maneno au tarakilishi,<br>• kutambua udogo katika maneno katika matini mbalimbali,<br>• kuandika majina ya vifaa vya darasani katika udogo (*k.v. kidawati, kijitabu*),<br>• kubadilisha nomino za hali ya wastani ziwe katika katika hali ya udogo akiwa na wenzake,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia hali ya udogo ipasavyo,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia nomino katika hali ya udogo akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la kuweka akiba,<br>• kuwasilisha kazi yake darasani ili wenzake wazitathmini,<br>• kumsomea mzazi au mlezi majina ya vitu vinavyopatikana nyumbani au | Je, ni mambo gani tunayozingatia tunapotumia nomino katika udogo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | shuleni katika udogo na kumtungia sentensi kwa kutumia maneno hayo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kujadiliana kuhusu udogo wa nomino.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua nomino katika hali ya udogo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia nomino katika hali ya udogo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino katika hali ya udogo na kuzitungia sentensi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake nomino katika hali ya udogo katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotumia udogo wa nomino kutunga sentensi kuhusu suala lengwa.
- Umaskini: mwanafunzi anapotumia udogo wa nomino kutunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya udogo wa nomino katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kuweka akiba na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Mathematics.

DRAFT

## 15.0 MAADILI YA KIJAMII

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **15.1.1 Usikilizaji Husishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya usikilizaji husishi,<br>b) kutambua vipengele vya usikilizaji husishi katika matini,<br>c) kujadili vipengele vya usikilizaji husishi ili kuvipambanua,<br>d) kushiriki mazungumzo akizingatia vipengele vya usikilizaji husishi,<br>e) kuchangamkia kushiriki katika kusikiliza husishi ili kuimarisha uwezo wa kufuatilia habari zinazoelezwa. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya usikilizaji husishi,<br>• kutambua miktadha rasmi na isiyo rasmi ambamo kusikiliza husishi hutokea katika jamii yake,<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza husishi (*k.v. kuwa makini, kuuliza maswali yasiyoelekeza, kuomba ufafanuzi, kumtazama mzungumzaji, kuelewa ujumbe anaotaka kukupitishia, kumhimiza kuzungumza badala ya kutoa ushauri, kutumia ishara zifaazo)* kutoka kwenye mazungumzo mafupi,<br>• kusikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa kutoka vifaa vya kidijitali kama vile vinasasauti na akizingatia, na kutambua vipengele vya kusikiliza husishi | 1. Je, ni miktadha gani rasmi na isiyo rasmi ambapo usikilizaji husishi hutokea?<br>2. Ni vipengele gani unazingatia katika kusikiliza husishi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vilivyozingatiwa,<br>• kuigiza vikao rasmi vya mazungumzo, *(k.v. kati ya mwalimu mkuu na mzazi kuhusu nidhamu ya mtoto)* akishirikiana na wenzake,<br>• kujadili vipengele vya kusikiliza husishi vilivyozingatiwa na wahusika katika mazungumzo hayo. | |

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake na kueleza kwa njia wazi miktadha rasmi na isiyo rasmi ambapo kusikiliza husishi hutokea.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia mazungumzo.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposikiliza na kuelezea hisia na maana za kauli za msemaji.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoeleza vipengele vya kusikiliza husishi anajenga ukakamavu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake na kujifunza zaidi vipengele vya kusikiliza husishi katika miktadha rasmi na isiyo rasmi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji; mwanafunzi anapoheshimu zamu ya wenzake katika mazungumzo.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

| |
|---|
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anaposikiliza matini kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha usikilizaji husishi katika somo la Kiswahili na usikilizaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.2 Kusoma** | **15.2.1 Ufupisho**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza kwa usahihi ujumbe wa aya za matini kwa sentensi mojamoja,<br>b) kueleza kwa usahihi ujumbe wa aya zote za matini kwa aya moja,<br>c) kuandika ufupisho unaozingatia mtazamo wa matini ya kufupishwa,<br>d) kufurahia kufupisha ujumbe kwa usahihi katika miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kujadili vipengele vya ufupisho *(k.v. habari muhimu katika aya, lugha ya anayefupisha, kudumisha mtazamo wa kifungu, idadi ya maneno),*<br>• kueleza kwa usahihi ujumbe katika kila aya kwa kutumia sentensi mojamoja,<br>• kueleza kwa usahihi ujumbe wa aya zote za matini kwa aya moja,<br>• kujadili kuhusu jinsi ya kuandika ufupisho wa matini,<br>• kuandika ufupisho unaozingatia mtazamo wa matini,<br>• kumsomea mzazi au mlezi ufupisho alioufanya ili autolee maoni. | Je, unazingatia nini unapofupisha kifungu cha ufahamu? |
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu ufupishaji wa kifungu.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma kifungu mtandaoni.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapoeleza jinsi ya kufupisha kifungu.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake jinsi ya kuandika ufupisho. | | | | |

DRAFT

| |
|---|
| • Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua aya za matini na kutambua hoja muhimu. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anaposikiliza maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushirikiana na wenzake kufupisha kifungu cha ufahamu.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anaposoma na kufupisha kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufupisho katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education. |

DRAFT

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.3 Kuandika** | **15.3.1 Baruapepe ya Kiofisi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaoafiki baruapepe ya kiofisi,<br>b) kutambua vipengele vya kimuundo vya baruapepe ya kiofisi,<br>c) kutumia lugha inayofaa katika uandishi wa baruapepe ya kiofisi,<br>d) kuandika baruapepe ya kiofisi kwa kuzingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao,<br>e) kujenga mazoea ya kuwasiliana kwa kuandika baruapepe ya kiofisi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua ujumbe unaoafiki baruapepe ya kiofisi,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya kimuundo vya baruapepe ya kiofisi ,<br>• kujadili na wenzake kuhusu lugha inayofaa katika uandishi wa baruapepe ya kiofisi,<br>• kuandika baruapepe ya kiofisi kwenye tarakilishi na kumsambazia mwenzake kupitia mtandao ili aitolee maoni,<br>• kumwandikia mwalimu wake baruapepe ya kiofisi ili aitathmini,<br>• kumsomea mzazi au mlezi baruapepe aliyoiandika ili aitolee maoni. | Je, ulizingatia vipengele gani katika baruapepe uliyowahi kuandika? |

| |
|---|
| **Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika baruapepe ya kiofisi na kuisambaza kwa mtandao.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika baruapepe ya kiofisi.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anpomsomea mzazi au mlezi wake baruapepe ya kiofisi. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji. |
| **Masuala mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapoandika baruapepe kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na masomo mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa baruapepe katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.4 Sarufi** | **15.4.1 Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini,<br>b) kujadili kanuni za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa kwa kuzingatia kanuni za kubadilisha usemi,<br>c) kutumia usemi halisi na usemi wa taarifa ifaavyo,<br>d) kuchangamkia matumizi ya usemi halisi na usemi wa taarifa katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini,<br>• kujadili kanuni za kubadilisha usemi *(k.v. wakati, nafsi, alama za uakifishi),*<br>• kutambua kanuni za kimsingi za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa,<br>• kubadilisha sentensi kutoka usemi halisi hadi usemi wa taarifa na usemi wa taarifa hadi usemi halisi,<br>• kutunga sentensi za usemi halisi na usemi wa taarifa akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la maadili ya kijamii,<br>• kuwasomea au kuwasambazia wenzake sentensi alizotunga ili wazitathmini. | 1. Usemi halisi unatofautianaje na usemi wa taarifa?<br>2. Unazingatia nini unapobadilisha usemi? |

DRAFT

**Umilisi wa kimsingi unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mwenzake sentensi sahili alizotunga za usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotunga na kutathmini sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa za wenzake.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapothamini maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii na kitaifa: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na masomo mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya usemi halisi na usemi wa taarifa katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya kijamii na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies na Religious Education.

DRAFT

## MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA

| **MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kusikiliza na kujibu ipasavyo** (*Mahojiano, maagizo, usikilizaji husishi, kusikiliza kwa makini*) | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia aina mbalimbali za kusikiliza na kujibu kwa wepesi. | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia aina mbalimbali za kusikiliza na kujibu. | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia baadhi ya aina za kusikiliza na kujibu. | Anasikiliza na kujibu ipasavyo akizingatia baadhi ya aina za kusikiliza na kujibu kwa kuelekezwa. |
| **kuweza kusikiliza na kufasiri ujumbe** *(Kutambua ujumbe, kuuhusisha ujumbe katika matini na maisha ya kila siku)* | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya kila siku kwa utendeti. | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya kila siku. | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya kila siku kwa kiasi. | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya kila siku kwa kiasi akielekezwa |
| **Kusikiliza kwa kina** (*Matamshi ya sauti mbalimbali: /**g**/, /**gh**/* /**ch**/ na /**sh**/) | Anasikiliza na kutambua sauti lengwa na kuzitamka kwa ufasaha. | Anasikiliza na kutambua sauti lengwa na kuzitamka. | Anasikiliza na kutambua baadhi ya sauti lengwa na kuzitamka. | Anasikiliza na kutambua baadhi ya sauti lengwa na kuzitamka akiongozwa. |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha** | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya aina | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya aina za |

| MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| *(Uzungumzaji wa papo kwa papo, uzungumzaji wa kutumia vidokezo)* | aina mbalimbali za uzungumzaji kwa ubunifu. | aina mbalimbali za uzungumzaji. | za uzungumzaji. | uzungumzaji akielekezwa. |
| **Kuweza kuwasilisha ujumbe na fani katika tungo za fasihi** *(Hadithi: mighani, visasili, hurafa, hekaya)* | Anawasilisha ujumbe na fani katika tungo mbalimbali za fasihi kwa ubunifu. | Anawasilisha ujumbe na fani katika tungo mbalimbali za fasihi. | Anawasilisha ujumbe na fani katika baadhi ya tungo za fasihi. | Anawasilisha ujumbe na fani katika baadhi ya tungo za fasihi kwa kusaidiwa. |

DRAFT

| MADA: KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu – Vifungu mbalimbali k.v. simulizi, mjadala, shawishi** *(ujumbe na msamiati)* | Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kutambua ujumbe na msamiati kwa utendeti. | Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kutambua ujumbe na msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu na kutambua ujumbe na msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu na kutambua ujumbe na msamiati kwa kiasi. |
| **Kuweza kusoma kwa kina.** *(Tamthilia: maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika, mbinu za lugha)* | Anasoma tamthilia na kutambua maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha kwa utendeti. | Anasoma tamthilia na kutambua maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha | Anasoma tamthilia na kutambua baadhi ya yafuatayo; maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha | Anasoma tamthilia na kutambua baadhi ya yafuatayo; maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha kina. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kusoma kwa mapana.** *(Kutambua na* | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua ujumbe na | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua vipengele | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua baadhi ya | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua baadhi ya |

| MADA: KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| *kuchagua matini ya kusoma*, *kutambua ujumbe, msamiati na matumizi ya lugha)* | matumizi ya lugha kwa mapana. | vinavyozingatiwa. | vipengele vinavyozingatiwa. | vipengele vinavyozingatiwa kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini.** | Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini kwa utendeti. | Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini. | Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha matini. | Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha matini kwa kuongozwa. |

| MADA: KUANDIKA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutumia viakifishi mbalimbali** *(alama ya hisi, ritifaa, mtajo, mshazari)* | Anatumia alama ya hisi, ritifaa, mtajo na mshazari kikamilifu na kwa wepesi. | Anatumia alama ya hisi, ritifaa, mtajo na mshazari kikamilifu. | Anatumia baadhi ya alama za kuakifisha kikamilifu. | Anatumia baadhi ya alama za kuakifisha kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha za kubuni.** (*Masimulizi, maelezo, mdokezo)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha za kiuamilifu.** (*Maelekezo, barua ya kirafiki ya kutoa shukrani, hotuba, barua ya kuomba msamaha, baruapepe ya kiofisi)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha za kiubunifu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | Anaandika aina mbalimbali za insha za kiubunifu kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |

DRAFT

| **MADA: SARUFI** | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili.** (*Aina mbalimbali za viwakilishi na vivumishi)* | Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa uketo. | Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi.** (*Hali ya mazoea, timilifu, wakati uliopita hali timilifu, wakati ujao hali timilifu)* | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi kwa uketo. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho** | Anatambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi | Anatambua viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi | Anatambua baadhi ya viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa | Anatambua baadhi ya viambishi vya ngeli, ngeli za nomino na kutumia kwa kiasi |

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango / Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **wa kisarufi ipasavyo.** (I – ZI, I – I, U – U na U – YA) | ipasavyo na kwa utendeti. | ipasavyo. | kisarufi ipasavyo. | upatanisho wa kisarufi ipasavyo. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya vitenzi na vielezi na kuvitumia katika matini.** | Anatambua vinyume vya vitenzi na vielezi na kuvitumia katika matini kwa ubunifu. | Anatambua vinyume vya vitenzi na vielezi na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya baadhi ya vitenzi na vielezi na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya baadhi ya vitenzi na vielezi na kuvitumia katika matini kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali.** *(Kutenda, kutendwa na kutendatenda)* | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali kwa wepesi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali. | Anatambua na kutumia vitenzi katika baadhi ya kauli. | Anatambua na kutumia vitenzi katika baadhi ya kauli kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia sentensi changamano.** | Anatambua na kutumia sentensi changamano katika matini kwa uketo. | Anatambua na kutumia sentensi changamano katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya sentensi changamano katika matini. | Anatambua na kutumia baadhi ya sentensi changamano katika matini kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya** | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na |

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango / Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **ukanushaji na kukanusha maneno kwa kuzingatia hali ya mazoea na timilifu.** | kwa kuzingatia hali ya mazoea na timilifu ipasavyo na kwa wepesi. | kukanusha kwa kuzingatia hali ya mazoea na timilifu ipasavyo. | kukanusha kwa kiasi kwa kuzingatia hali ya mazoea na timilifu ipasavyo. | kukanusha kwa kiasi kwa kuzingatia hali ya mazoea na timilifu kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo.** | Anatambua na kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo kwa ufasaha. | Anatambua na kutumia nomino katika hali ya ukubwa na udogo. | Anatambua na kutumia baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa na udogo. | Anatambua na kutumia baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa na udogo akielekezwa. |
| **Kuweza kutumia usemi halisi na usemi wa taarifa.** | Anatumia usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu kwa wepesi. | Anatumia usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu | Anatumia kwa kiasi usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu. | Anatumia kiasi usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kwa kuongozwa. |

## MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI

Katika Gredi Nane, wanafunzi watashiriki katika mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji kwa kuchagua kutoka somo moja au kwa kuunganisha masomo mbalimbali. Mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji utawawezesha mwanafunzi kutumia maarifa na ujuzi kutoka kwa masomo mengine kushughulikia tatizo katika jamii. Utekelezaji wa mradi huu wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji utachukua Mtazamo Kamili wa Shule, ambapo wanachama wote wa jamii ya shule ikiwa ni pamoja na walimu, utawala wa shule, wazazi/walezi/ jamii na wafanyakazi wengine wa shuleni. Itakuwa jitihada za ushirikiano ambapo mwalimu wa Somo la Kijamii (Social Studies) anaratibu na kufanya kazi na walimu wengine wa masomo mbalimbali kubuni na kutekeleza miradi ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji pamoja. Walimu watachagua mada kutoka kwa masomo mbalimbali na mada tofauti tofauti za masuala mtambuko kwa mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Pia inapaswa kutoa fursa ya ukuzaji wa umilisi wa kimsingi na maadili. Wanafunzi watashiriki katika mradi mmoja wa pamoja wa darasa wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji uliounganishwa ukifuata hatua sita za maendeleo kama ifuatavyo:

| **Hatua** | **Maelezo** |
|---|---|
| **Hatua ya 1** | **Utambuzi wa Tatizo**<br>Wanafunzi wanachunguza jamii yao ili kuelewa changamoto zinazokabiliwa na athari zake kwa wanajamii. Baadhi ya changamoto katika jamii zinaweza kuwa:<br>● Uharibifu wa mazingira<br>● Magonjwa ya mienendo ya maisha, magonjwa ambukizi na yasiyoambukizwa<br>● Umaskini<br>• Misukosukona migogoro katika jamii<br>• Uhifadhi wa vyakula |

| | |
|---|---|
| **Hatua 2** | **Kubuni Suluhisho**<br>Wanafunzi wanabuni njia ya kuingilia kati kushughulikia changamoto iliyotambuliwa. |
| **Hatua 3** | **Mpango wa Mradi**<br>Wanafunzi wanagawana majukumu, kutengeneza orodha ya shughuli zitakazofanywa, kuandaa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kutekeleza mradi, na kuweka ratiba za utekelezaji. |
| **Hatua 4** | **Utekelezaji**<br>Wanafunzi wanatekeleza mradi na kuweka idhibati wa kazi iliyofanywa. |
| **Hatua 5** | **Kuonyesha Mradi na Kuandika Ripoti**<br>Maonyesho ni pamoja na kuonyesha vitu vya mradi wa wanafunzi kwa jamii na kutafakari kuhusu maoni wanayopokea.<br>Wanafunzi wanandika ripoti inayoelezea shughuli za mradi wao na mafunzo waliyopata kutokana na maoni waliyopewa. |
| **Hatua 6** | **Tafakuri**<br>Wanafunzi wanapitia kazi yote ya mradi kujifunza kutokana na changamoto walizokutana nazo. Wanahusisha kazi ya mradi na dhana za masomo, wakiangazia jinsi dhana hizo ziliwasaidia kutekeleza mradi pamoja na jinsi mradi ulivyosaidia kuimarisha uelewa wao wa dhana za masomo. |

**TANBIHI**: Hatua hizi zitapangwa kwa muda katika mihula mitatu ya kalenda ya masomo.

**Tathmini ya miradi ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji**

Tathmini kwa ajili ya mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji uliounganishwa utafanywa kwa njia ya tathmini ya mara kwa mara. Tathmini itazingatia mchakato na matokeo ya mwisho. Hii inajumuisha kutathmini kila hatua ya

maendeleo ya mradi wa darasa wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Itatazama vipengele vitatu, yaani: ujuzi kutoka masomo mbalimbali uliotumika katika kutekeleza mradi, umilisi wa kimsingi uliokuzwa, na maadili yaliyokuzwa.

DRAFT

## MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI

| Mada | Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| **Kusikiliza na Kuzungumza** | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi kufanyiana tathmini | • Chati<br>• Michoro na picha<br>• Mgeni mwalikwa<br>• Vifaa vya kidijitali (k.v tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>• Mti maneno<br>• Kapu maneno<br>• Vitabu mbalimbali | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Kusoma** | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni |

| Mada | Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| | b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kusoma kwa sauti<br>e) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>f) Potifolio<br>g) Shajara | • Rununu<br>• Projekta<br>• Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• Kamusi mbalimbali | 3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Kuandika** | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potifolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | • Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Kielelezo cha insha ya wasifu<br>• Nakala ya barua ya kirafiki<br>• Nakala ya barua rasmi | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Sarufi** | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu | 1. Kazi ya vikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani |

DRAFT

| Mada | Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| | lengwa<br>c) Kujaza mapengo<br>d) Kutunga sentensi<br>e) Kazi mradi | • Projekta<br>• Kapu maneno<br>• Mti maneno<br>• Kadi maneno<br>• Picha za vitu mbalimbali<br>• Michoro<br>• Chati<br>• Mabango<br>• Sanamu<br>• Nyenzo halisi | 4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |